


**YAMAL AVUNJA REKODI YA MIAKA 77 CLASICO**

UKURASA 21

**SIKU 18** hakuna usafiri wa maji Mafia, serikali kuunda timu

UKURASA 5

**DEREVA** adakwa akiendesha basi kwa kutumia leseni ya pikipiki

UKURASA 10

**UINGEREZA** yabanwa kulipa fidia biashara ya utumwa iliyofanya

UKURASA 19

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatatu Oktoba 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581843

www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Tembo wavamia makazi, wenyeji wafunga barabara



**MAGARI** yakwama kwa saa mbili; wamwibua DC, mbunge kwenda kuwasihi... *Endelea ukurasa wa 2*




## RIPOTI MAALUMU

# Wagombea wanawake: Tunadhalilishwa mitandaoni, tunabaki wanyonge kisiasa

UKURASA 4



# Samia: Viongozi wa dini milango iko wazi, njooni tujadili mezani

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA HAITAKI KUPOA, YAVUTA KIUNGO UTURUKI UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Wananchi wafunga barabara kushinikiza tembo kuondolewa

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WANANCHI wa Kijiji cha Mkiwa, wilayani Ikungi, mkoani Singida, wamefunga barabara kuu ya Dodoma - Singida kwa magogo ya miti kwa zaidi ya saa mbili, wakishiniza serikali ichukue hatua za kuwaondoa tembo waliovamia eneo hilo na kubomoa nyumba na kula mazao.

Wakizungumza na Nipashe jana eneo la tukio, baadhi ya wananchi hao walisema kundi la tembo hao lilivamia makazi yao juzi saa 10 jioni na kubomoa nyumba zao na kula vyakula, hali iliyoleta taharuki kubwa kijijini, wakazi wakikimbia ovyo.

Ramadhani Ally, mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, alisema tembo hao wameharibu miti na shamba la mihogo na kubomoa nyumba yake.

Halima Shaban, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alisema wameamua kufunga barabara hiyo, kushinikiza serikali ichukue hatua kwa kuwa mara kadhaa tembo wamekuwa wanavamia kijiji hicho na kufanya uharibifu wa nyumba na mashamba.

"Tembo wamekuwa wakivamia makazi na hakuna kinachofanywa na serikali kuwadhibiti, kila mara tembo hawa wanatuharibia vitu na kutuacha masikini, sasa tumechoka," alitamka kwa hasira.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, walifika eneo la tukio kuwatuliza wananchi hao ambao kutokana na kufunga barabara hiyo, walisababisha msongamano mkubwa wa magari na kuleta usumbufu kwa abiria. Mtaturu aliwaeleza wananchi hao kuwa kijiji na kata nzima ya Mkiwa na Isuna ni mapito ya tembo, hivyo inakuwa ngumu kuwazuia na kwamba serikali imekuwa inachukua hatua kuwadhibiti.

"Maliasili tunazihitaji na wanadamu tunawahitaji, niwaombe jitihada zinafanywa na serikali, hakuna makusudi yanafanyika katika kushughulikia suala hili.


"Nitampigia simu Waziri wa Maliasili na Utalii (Balozi Dk. Pindi Chana), muda huu, ili aje yeye au awatume wawakilishi kuja kushughulikia suala hilo," alisema.

Awali, mbunge huyo pia alimweleza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, kwenye kikao cha majumuisho ya ziara yake ya siku tano mkoani Singida, kwamba tembo hao wamevamia makazi katika vijiji vya kata za Mkiwa na Isuna.

Mara kadhaa tembo wamekuwa wanasababisha uharibifu wa mashamba na wakati mwingine kusababisha vifo kwa wananchi katika wilaya ya Ikungi, ambako makundi ya tembo yamekuwa yakipita kuelekea pori la akiba la Ruangwa lililoko Itigi, wilayani Manyoni.

Ni ishara ya kuwapo uvamizi katika shoroba za wanyamapori nchini.

Ndovu huwa hawasahau eneo ambako wao wenyewe walipita zamani, watangulizi (wazazi au ukoo wao) walipita awali, hata kama ni miaka 1,000 imepita.




Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda (kushoto), akabidhi zawadi kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Baobab, iliyoibuka Mshindi wa Jumla katika shindano la Vilabu vya Kodi kwa Shule za Sekondari za Dar es Salaam na Pwani, zawadi kadhaa ikiwamo Printer kubwa, fedha taslimu ya shilingi milioni saba, zilitolewa katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Chuo cha Kodi (ITA), Mikocheni, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia: Viongozi wa dini milango iko wazi, tujadiliane meza moja

**Na Mwandishi wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, yuko tayari kuendelea kushirikiana na viongozi wa dini kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu ustawi wa nchi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alitoa kauli hiyo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akimwakilisha Rais Samia katika ibada maalumu ya shukrani ya kuadhimisha miaka 50 ya Pastoreti ya AICT Magomeni.

"Rais anakumbuka namna mnavyomshirikisha katika masuala mbalimbali yanayohusu kanisa na kwa kweli milango yake iko wazi, anawakaribisha wakati wowote, ili mtoe maoni yenu ya namna ya tunavyoweza kuongoza nchi yetu," alisema Dk. Biteko.

Vilevile, alisema maadhimisho ya jubilee ni kukumbuka wakati uliopita na kuangalia eneo gani lilifanyiwa kazi vizuri na lipi halikufanyiwa.

Aliwahimiza waamini wa kanisa hilo kujitoa kwa hali na mali katika kujenga bila kusubiri kesho. "Wito wangu kwetu, tusiangalie leo, tuangalie miaka 200 kanisa hili litakuwa wapi, tusisubiri kesho kwa kuwa hatujui. Fanya chochote unachoweza kufanya leo," alisisitiza.

Dk. Biteko alitoa wito kwa kanisa hilo kuendeleza umoja miongoni waumini wake na Watanzania kwa ujumla na kusema kuwa wafuate misingi ya uazilishwaji wake ambayo ni kujitawala, kujiendesha na kujieneza.

"Hubirini upendo na msiruhusu mtu kutugawa wala kutubagua, Mungu ametupa nchi nzuri yenye rasilimali za kutosha. Niwaombe maaskofu na wachungaji wa kanisa hili, msivunjike moyo.

"Kusudi mliloitiwa na Mungu, lisimamieni na waumini wa kanisa hili tuwe sauti nzuri, tuwasaidie viongozi wetu na tuwatie moyo," alisisitiza Dk. Biteko.

> **"Rais anakumbuka namna mnavyomshirikisha katika masuala mbalimbali yanayohusu kanisa na kwa kweli milango yake iko wazi, anawakaribisha wakati wowote, ili mtoe maoni yenu ya namna ya tunavyoweza...**

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Naibu Waziri Mkuu huyo, alipongeza Kanisa la AICT kwa kuendelea kutoa hamasa kwa jamii na kuwakumbusha Watanzania kushiriki uchaguzi huo na kuchagua viongozi wenye sifa.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Mkuu, Musa Magwesela, alisema ibada hiyo ni muhimu kwa kuwa tangu kanisa hilo lianzishwe Magomeni mwaka 1974, limekuwa na mchango muhimu katika kutangaza injili.

"Kuna sababu 14 za kuhubiri utukufu na maajabu ya bwana, kanisa hili la Magomeni kwa mujibu wa Zaburi 96 tumetumia njia 12 kuhubiri jina la bwana, ikiwamo kutumia nyimbo," alisema Askofu Magwesela.

Aliongeza kuwa wakristo wamehimizwa kutenda matendo mema, kutumia vipaji na kutumia karama.

Alisema kanisa linatambua michango ya watu mbalimbali waliyotoa wakati wanafanya kazi katika kanisa hilo la Magomeni, huku akitaja majina ya baadhi ya wachungaji waliohudumia kanisa hilo.

"Wito wangu, tuenzi michango ya waliohubiri utukufu na maajabu ya Bwana," alisema Askofu Magwesela.

Vilevile, katika kuunga mkono jitihada za Rais Samia, Askofu Magwesela alisema kuwa Oktoba 26, mwaka huu, kanisa hilo liligawa mitungi 20 ya nishati safi ya kupikia kwa jamii inayolizunguka kanisa.

Sambamba na ibada hiyo, kanisa hilo limeendesha harambee, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kanisa, ofisi na madarasa ya watoto, Rais Samia akichangia Sh. milioni 100.

HABARI KITAIFA

# TCRA: Huduma za kidijitali zinazidi kuwafikia wengi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya Mawasiliano Tanzania, imeendelea kuimarika ndani ya miezi mitatu kutokana na kuenea huduma zinazotumia teknolojia za kidigitali katika maeneo mengi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, aliyasema hayo jana, wakati akizungumzia ukuaji wa mawasiliano nchini.

Alisema kuenea kwa teknolojia na vifaa vya watumiaji miongoni mwa watu kuliongezeka kwa kati ya pointi moja na tatu kati ya Juni na Septemba, 2024.

"Huduma zinazowezeshwa na teknolojia za juu zaidi pia zimeongeza kasi ya intaneti, zimewezesha mitandao kuimarika na kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Teknolojia zimeongeza ubora wa huduma.

"Teknolojia za simu za mkononi uzao wa tatu (3G) zimezidi kuenea kwa watu, kutoka asilimia 89 hadi 90.1. uzao wa nne (4G) umeenea zaidi kutoka asilimia 83 hadi 84.9 na wa tano (5G) kutoka asilimia 15 hadi 18," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kijiografia, 4G imeenea asilimia 73.6 kutoka asilimia 73 na 4G kwa asilimia 70.2 kutoka asilimia 69. Uzao wa tano kijiografia umeenea asilimia 2.2 Septemba 2024 kutoka asilimia mbili Juni mwaka huu.

"Teknolojia hizi zinawezesha huduma za maongezi, ujumbe mfupi (meseji) na intaneti. Teknolojia ya 5G ambayo iliingia Tanzania mara ya kwanza mwaka 2022, ina kasi kubwa ya intaneti, inapunguza ucheleweshaji kusafirisha data na inaunganisha watumiaji na mitandao kwa ufanisi zaidi," alisema.

> **"Teknolojia za simu za mkononi uzao wa tatu (3G) zimezidi kuenea kwa watu, kutoka asilimia 89 hadi 90.1. uzao wa nne (4G) umeenea zaidi kutoka asilimia 83 hadi 84.9 na wa tano ...**

Dk. Jabir alisema taarifa hiyo imeeleza kwamba simu zenye uwezo mkubwa au simu janja. zimeenea miongoni mwa watu, kwa asilimia 33.85 kutoka asilimia 31.5 Juni 2024.

"Simu janja zina programu tumizi changamani zaidi na zinawezesha intaneti ya kasi. Watumiaji intaneti Tanzania wameongezeka kwa asilimia tano kati ya Julai na Septemba 2024 kutoka milioni 39.3 hadi 41.4," alisema.

Alisema watumiaji wanakokotolewa kutokana na laini za siku zilizotumika kutoa huduma ya intaneti ndani ya miezi mitatu iliyotangulia kwa kutumia teknolojia yoyote ile.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, huduma za intaneti zinapatikana zaidi kupitia vifaa vya mkononi na visivyo na waya. Taarifa inaonesha asilimia 99.7 ya watumiaji intaneti walipitia teknolojia za vifaa vya mkononi.

"Matumizi ya data yameongezeka kutoka wastani wa megabaiti (MB) 4.647 kwa mtumiaji Juni mwaka huu hadi MB 4.855 Septemba, 2024," alisema.

Aliongeza kuwa wastani wa kasi ya kupakia data kwa watumiaji vifaa vya mkononi vinavyowezesha intaneti ya kasi, unaopimwa kwa megabaiti moja kwa sekunde (Mbps), uliongezeka kutoka Mbps 11.4 Juni hadi 13.3 Septemba, 2024.

# Mkemia awaonya waagizaji rangi kuzingatia maelekezo

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kupitia Kituo cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, kimewataka wazalishaji na waingizaji rangi nchini, kuzingatia maelekezo waliyopewa, ili kudhibiti sumu itokanayo na madini ya risasi.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka GCLA, Daniel Ndiyo, wakati wa mkutano wa wadau wa rangi uliolenga kuimarisha ushirikiano kwa pande zote mbili.

Alisema lengo ni kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya rangi, ili kulinda usalama wa watumiaji kutokana na athari za kemikali hiyo.

"Rangi ina sumu inayotokana na madini ya risasi. Endapo ikitumika kupaka kwenye mabati katika kipindi cha mvua na watu hutumia maji hayo, bila kuwa na uhakika wa usalama wake, maji wanayokinga kutoka kwenye mabati ni wazi watapata madhara," alionya.

Alisema hatua hiyo imewafanya kuendelea kutoa elimu kwa wadau wanaohusika na kemikali nchini, kufuata kanuni na taratibu zote zilizowekwa na mamlaka, kwa ajili ya usalama wao na kulinda afya za watanzania.

Alitoa rai kwa wadau wanaohusika na eneo hilo, kuondokana na dhana potofu ambayo imezoeleka, kutumia maziwa pekee, kwa ajili ya kudhibiti sumu mwilini kwa sababu inaweza kudhibiti baadhi ya sumu chache pekee na si zote kama inavyodhaniwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaalamu ya Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Prof. Amos Mwakigonja, aliwaagiza wadau wanaoshughulika na kazi zinazohusiana na madini ya risasi, kuunga juhudi zinazofanyika kwa kuachana na shughuli zinahusiana na usambazaji madini hayo katika mazingira; kutasaidia kuepusha madhara kwa wananchi.







**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

## TAARIFA KWA UMMA

## NAMBA MPYA YA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inapenda kuwafahamisha wadau wote na Umma kwa ujumla kwamba kufuatia maoboresho iliyoyafanya katika Kituo chake cha Huduma kwa Wateja (Call Centre), namba ya simu ya Huduma kwa Wateja itakayokuwa ikitumika ni ya Kampuni ya simu ya Tanzania (TTCL) ambayo ni: **023 – 221 0500.**

Kwa muktadha huo, namba zote zilizokuwa zikitumika kuwasiiana na Kituo chetu hicho cha Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kuulizia masuala mbalimbali yahusuayo Usajili na Utambuzi wa watu ikiwa ni pamoja na kufahamu kuhusu Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) na Vitambulisho vya Taifa, zitafungwa rasmi kuanzia tarehe 28/10/2024 na badala yake namba itakayotumika ni hiyo iliyotajwa hapo juu.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Mawasiliano na Hifadhi Hati**

**Barabara ya Kilimani, S.L.P 12324, Dar es Salaam, Simu: +255734220962, Barua pepe: info@nida.go.tz, Tovuti: www.nida.go.tz**

# Wagombea wanawake: Tunadhalilishwa mitandaoni, tunabaki wanyonge kisiasa

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya wanawake waliojitosa kuwania uongozi wa kisiasa, wamesema walikumbana na udhalilishaji mtandaoni, wakiitaja mitandao ya kijamii kuwa "sumu kwa wanawake kisiasa".

Kinamama hao wamesisitiza kuwa aina hiyo ya udhalilishaji ni miongoni mwa mambo yanayorudisha nyuma mikakati ya kitaifa inayolenga kufikia usawa wa kijinsia katika siasa, takwimu rasmi za kiserikali zikionesha kundi hilo bado halina uwakilishi ukubwa katika vyombo vya uamuzi.

Ni ukatili ambao wamedai haufanywi kwa kutokujua, bali ni mikakati ya makusudi ya baadhi ya watu kudhoofisha ushiriki wa wanawake kisiasa kwa kuwatia woga na kuwakatisha tamaa kushiriki katika siasa.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Kitaifa ya Kidemokrasia (NDI), katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, wanawake waliochaguliwa kwa nafasi za ubunge ni asilimia 9.5, wabunge wa viti maalumu ni asilimia 29, hivyo kufanya jumla ya wabunge wanawake kuwa 142 kati ya 393.

Vilevile, ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ya mwaka 2020 inaonesha wanawake waliochaguliwa kwa nafasi za udiwani walikuwa asilimia 6.58 (260 kati ya madiwani 3,953), viti maalum walikuwa 1,374 katika halmashauri 184 sawa na asilimia 24.59. Kwa jumla, wanawake walikuwa asilimia 29.24 ya madiwani wote nchi nzima.

Ripoti ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019 pia inaonesha kuwa kati ya nafasi 11,915 za wenyeviti wa vijiji, wanawake walishinda nafasi 246 sawa na asilimia 2.1, huku wanaume wakishika asilimia 97.9 ya nafasi hizo. Kati ya nafasi 4,171 za wenyeviti wa mitaa, wanawake walishinda nafasi 528 sawa na asilimia 12.6.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Tanzania Bara, Magdalena Sakaya, anasema udhalilishaji wanawake mtandaoni unachangia kulikatisha tamaa kundi hilo kuingia katika ulingo wa siasa.

Magdalena anaeleza alivyokumbana na changamoto hiyo katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 alipogombea Ubunge wa Kaliua, mkoani Tabora, akidai kuwa wapinzani wake waliwatuma watu wakarekodi lugha za matusi na kuambatanisha na picha zake kisha kuzisambaza katika mitandao ya kijamii ya Facebook na WhatsApp.

"Kama mbunge nilipitia hali hiyo, wanachukua video za michango yako ulipokuwa unatoa bungeni na kuunganisha na lugha za matusi yaliyokuwa yanatolewa kwenye majukwaa ya kampeni. Mashambulizi haya yanasambazwa kimkakati kiasi kwamba ni vigumu kuyahusisha moja kwa moja na mpinzani wako," anasema.



Waziri Dorothy Gwajima

Magdalena anaendelea kusimulia madhila aliyopita, akieleza kuwa miaka miwili iliyopita, yaani mwaka 2022 muwewe alitumiwa kipande cha video kwa njia ya WhatsApp kikimwonesha yeye (Magdalena) akiwa na bosi wake kichama wakiwa kwenye hafla ya chama.

"Mtu aliyemtumia video hiyo alidai kwamba mimi nina uhusiano wa kimapenzi na Mwenyekiti wa Taifa wa CUF na kwamba hiyo ndio sababu ya kuteuliwa kwangu kuwa Naibu Katibu Mkuu wa chama," anasimulia.

Magdalena anazitaja ni tuhuma zilizomwumiza na kuna wakati alipata hisia za kukata tamaa kuendelea na siasa, ikizingatiwa kuwa mumewe alikaa na jambo hilo kwa muda mrefu bila kumwuliza chochote hadi siku walipokuwa wanazungumza namna mazingira ya siasa yalivyo magumu kwa wanawake.

"Mume wangu aliendelea kubaki kimya hadi nilipozungumzia jinsi mazingira ya siasa yanavyoweza kuwa sumu.

"Vitendo hivi vinawakatisha tamaa wanawake kushiriki katika siasa, kwani ujumbe wa mitandao ya kijamii unaweza kuwafikia watu wengi, wakiwamo watoto wako, mwenzi wako, wazazi wako, wafanyakazi wenzako kazini na hata viongozi wa kidini.

"Mambo haya yanawafanya watu kuogopa na kuona kuwa siasa zitaacha doa kwao, hivyo kuwa kikwazo kikubwa kufikia uwakilishi wa 50/50," Magdalena anatoa angalizo.

Anapendekeza kutungwa sheria zinazoharamisha maneno ya chuki, matusi na mashambulizi wakati wa kampeni, akitaka yeyote anayehusika na vitendo hivyo apigwe marufuku kushiriki uchaguzi.

Shamila Makwenjula (50), anajitambulisha ni miongoni mwa waathirika wa udhalilishaji huo, akidai kuwa mitandao ya kijamii ilitumika kumdhalilisha alipogombea uenyekiti wa kijiji cha Mtimbila, mkoani Morogoro mwaka 2019.

Wakati wa kampeni, Shamila anasema alipokea mfululizo wa ujumbe kupitia mitandao ya kijamii ya WhatsApp na Facebook kutoka kwa baadhi ya watu, wakimkejeli kuwa "umeshindwa kuzaa, utawezaje kuongoza kijiji".

"Baadhi ya machapisho hayo yalinidhalilisha sana. Walinihoji sifa zangu za uongozi, wakisema, 'Huna mtoto, utawezaje kuwa kiongozi? Huna mtoto unataka kumtetea nani? Hukumzalia mume wako mtoto, hatuna nafasi kwa wanawake tasa katika kijiji chetu'," ananukuu sehemu ya ujumbe aliotumiwa.

Anasema licha ya kupitia changamoto hizo, hakukata tamaa. Mwaka 2020 aliamua kugombea udiwani kata ya Mtimbila. Unyanyasaji dhidi yake uliendelea, baadhi ya wakazi wa eneo hilo, hasa katika kijiji anachotoka, walimshambulia kwa maneno hayo ya udhalilishaji.

Utafiti uliofanywa na Umoja wa Mabunge ya Afrika (APU) mwaka 2021, ukihusisha wabunge wanawake 224 kutoka nchi 50, ikiwamo Tanzania, ulibaini kuwa asilimia 80 ya waliohojiwa walipitia ukatili wa kisaikolojia, huku asilimia 46 wakikumbana na ukatili wa kijinsia mtandaoni.

Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2023, inaonesha kuwapo ongezeko kubwa la udhalilishaji wa kidijitali na ukatili wa kijinsia mtandaoni nchini, wanawake wakiwa walengwa wakuu, kwa asilimia 56.

Katika ripoti yake hiyo, LHRC ina lingine la ziada kwamba licha ya unyanyasaji huo, wanawake hawatafuti msaada wa kisheria. Ripoti yake inaonesha kuwa asilimia 65 ya wateja waliotembelea kituo mwaka huo walikuwa wanaume.

LHRC inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Anna Henga, inabainisha katika ripoti yake kuwa unyanyasaji huo unasababisha wanawake kujitenga na matumizi ya mitandao ya kijamii, ripoti ya kituo ikionesha kwamba wanaume ndio watawala wakuu wa mitandao hiyo.

Ripoti ya LHRC inaonesha kuwa kwenye majukwaa kama Twitter (sasa X), wanaume wanachukua asilimia 80 ya watumiaji wanaopata taarifa zinazohusiana na msaada wa kisheria na haki.

Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Doroth Semu, hayuko mbali na hoja hiyo. Anasema kukua kwa matumizi ya mitandao ya kijamii kumegeuka kuwa anguko la harakati za kisiasa kwa wanawake kwa kuwa hutumika kama silaha ya kuwakatisha tamaa.

"Wanawake wanasiasa wanapokuwa wanaweka kazi zao za kisiasa kwenye mitandao ya kijamii, badala ya kutiwa moyo, wanapokea lugha za matusi, maneno ya karaha na udhalilishaji. Inawavunja nguvu kushiriki siasa.

"Kuna idadi kubwa ya wanasiasa kwenye mitandao ya kijamii, lakini wanaitumia kuweka mambo tofauti na siasa kwa kuogopa matusi. Matokeo yake jamii haioni harakati zao na mambo makubwa wanayoyafanya, hivyo ikifika kipindi cha uchaguzi hawawapigii kura," anasema.

Anashauri wanawake wanasiasa kufanya alichokiita "kuvaa ngozi ngumu" ili kutoruhusu maneno hasi kuwavuruga.

Mkurugenzi Mkuu wa Tech & Media Convergency (TMC), Asha Abinallah, anasema kuwa mwaka 2022 walifanya utafiti juu ya hali ya unyanyasaji wa kijinsia mtandaoni kwa wanawake viongozi katika siasa. Utafiti huo uliokusanya maoni ya zaidi ya wanawake 340.

Anasema matokeo yalionesha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya viongozi hao wanawake walikuwa wameacha kutumia mitandao ya kijamii kutokana na unyanyasaji wa kijinsia.

Ni matokeo yaliyosukuma TMC kuja na mpango wa kutoa mafunzo ya namna ya kutumia zana za mitandao ya kijamii kwa ufanisi, kujilinda mtandaoni na kujenga uhimilivu wa kidijitali, hasa kwa wanawake ambao tayari wanatumia mitandao ya kijamii.

"Kwa miezi minne, tulifanya majadiliano ya vikundi, ili kuelewa changamoto wanazokutana nazo wanawake na kuwapa elimu ya jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo.

"Pia tulijifunza mengi kutokana na uzoefu wao. Hadi sasa, programu hiyo imewafikia moja kwa moja zaidi ya wanawake 450 kupitia majukwaa mbalimbali, mijadala, na vikundi vya majadiliano," anasema Asha.

Msaikolojia Tiba, Saldeen Kimangale anataja athari za kisaikolojia zinazotokana na unyanyasaji mtandaoni kuwa ni pamoja na kuwa na wasiwasi, huzuni na hata kujidhuru kwa kuwa mashambulizi hayo yanakusudia kuwanyamazisha na kuwabagua waathirika, wakiwanyima nafasi ya kushiriki katika maeneo ya kidijitali kwa uhuru.

Wakili wa Mahakama Kuu Tanzania na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-TAN), James Marenga, anawashauri wanasiasa wanawake kuwafungulia mashtaka wale wanaowadhalilisha mitandaoni, akisisitiza kuwa unyanyasaji wa kidijitali kupitia maandishi, picha au video unaweza kushughulikiwa kisheria.

Anasema Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2014 imeweka wazi kuwa ni kosa kutumia vifaa vya kielektroniki kuwanyanyasa wengine. Pia Inakataza kusambaza ujumbe wa kashfa na picha za ponografia na inaungwa mkono na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) ya Mwaka 2010.

Anawashauri wanasiasa wanawake kuhifadhi ushahidi wote wa kidijitali, ikiwa ni pamoja na maandishi, picha na video, ili kujenga kesi imara ya kashfa au unyanyasaji mahakamani, hata kupinga matokeo ya uchaguzi au kudai fidia inapobidi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dorothy Gwajima, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi unaojulikana kama "Women Now" unaotekelezwa na Taasisi ya Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) Septemba 19, mwaka huu, alisisitiza wanawake wanaokumbana na ubaguzi au unyanyasaji wakati wa kampeni za nafasi za uongozi, wana haki ya kutafuta haki kisheria.

Alisema Kifungu cha 135 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, kinatambua unyanyasaji wa wanawake katika siasa kama kosa la uchaguzi.

Sheria tajwa inaelekeza kuwa: "Mtu yeyote ambaye kwa makusudi ya kusababisha shambulio la kijinsia la aibu kwa kutoa maneno au sauti, kuonesha vitendo au kutoa maneno, au kuonesha ishara yoyote ambayo itaonekana na mtu mwingine atakuwa ametenda kosa la shambulio la kijinsia na akipatikana na hatia atawajibika na kifungo kisichozidi miaka mitano au faini isiyozidi laki tatu (Sh. 300,000) au vyote viwili, kifungo na faini."

# Mafia yakosa huduma vivuko siku 18, serikali kuunda timu

**Na Julieth Mkireri,** MAFIA

ZIKIWA zimefika siku 18 bila kuwa na usafiri vivuko katika wilaya ya Mafia, mkoani Pwani, serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, imesema itaundwa timu maalumu itakayosimamia urejeshwaji huduma hiyo.

Timu hiyo itahusisha Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ulinzi na itashirikiana na timu ya mkoa wa Pwani kushughulikia tatizo hilo ambalo limesimamisha baadhi ya shughuli za wakazi wa wilaya hiyo.

Vivuko vya MV Kilindoni na MV Songosongo, vinavyofanya safari kati ya vituo vya Mafia na Nyamisati (Kibiti) vimesimamisha huduma ya usafiri huo tangu Oktoba 10, mwaka huu.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa wilayani Mafia, mkoani Pwani wakati akikagua matengenezo ya Kivuko cha MV Songosongo kinachosimamiwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ) kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Waziri Bashungwa alieleza kuwa serikali inatambua umuhimu wa huduma ya usafiri wa vivuko katika wilaya ya Mafia, ambayo shughuli zake nyingi zimesimama kutokana na vivuko vya MV Kilindoni na MV Songosongo kupata hitilafu. Matengenezo yanaendelea kwa vivuko vyote wiwili.

"Serikali ipo kazini na kupitia timu hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, itafanya jitihada za haraka za kurudisha huduma ya vivuko viwili vya MV Songosongo na MV Kilindoni, ili kuwaondolea adha wana Mafia ya kukosa usafiri wa vivuko", alisema Bashungwa.

Waziri huyo alisema mkakati wa serikali ni kuongeza kivuko kingine, ili kusaidia wakati wa dharura kwa kutoa huduma kwa wananchi pindi kivuko kingine kinapopata hitilafu.

Vilevile, Waziri Bashungwa aliwahakikishia wananchi wa Mafia kuwa timu hiyo ya wataalamu itafanya kazi usiku na mchana, kuhakikisha wanarejesha huduma za vivuko haraka iwezekanavyo.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema ofisi yake inaendelea kuongeza na wawekezaji wa sekta binafsi watakaoweza kufanya uwekezaji wa huduma ya usafiri na hoteli, ili kushirikiana na serikali katika utoaji huduma hizo ambazo zitaendelea kufungua uchumi wa wilaya ya Mafia.

# CRDB yatunukiwa tuzo za 'Benki Bora' na 'Benki Salama Tanzania'

**WASHINGTON D.C,**

MAREKANI

BENKI ya CRDB imetambuliwa kwa mara nyingine kama kinara katika sekta ya benki Tanzania, kwa kushinda tuzo za 'Benki Bora Tanzania' na 'Benki Salama Tanzania' zilizotolewa na Jarida la Global Finance, wakati wa hafla ya 31 ya Mwaka ya Tuzo za Benki Bora.

Tuzo hizo zilitolewa juzi katika hafla iliyofanyika sambamba na mikutano ya mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB), huko Washington D.C, Marekani.

Hii ni mara ya tano mfululizo kwa Benki ya CRDB kushinda tuzo ya Benki Bora Tanzania na mara ya pili mfululizo kwa Benki Salama Tanzania - ikidhihirisha uimara wa benki hiyo katika sekta ya fedha.

Mafanikio hayo yanadhihirisha mkakati wa benki hiyo wa kukua kwa njia endelevu inayowanufaisha wateja, wawekezaji na uchumi wa Tanzania kwa ujumla.

Vilevile, tuzo hizo ni kielelezo cha uongozi thabiti wa Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Group, Abdulmajid Nsekela na zinadhihirisha mchango wa Benki ya CRDB katika kuimarisha sekta ya fedha Tanzania na ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kati.

"Tunajivunia sana kwa kutambuliwa kwa mara nyingine kama Benki Bora Tanzania na Benki Salama katika tuzo za Global Finance.

"Tuzo hizi ni ishara kwamba tupo kwenye njia sahihi ya ukuaji - kutoa huduma za kipekee kwa wateja wetu, thamani kwa wanahisa wetu na kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya fedha nchini," alisema Nsekela.

Benki ya CRDB imekuwa na mwaka wa mafanikio makubwa kutokana na maboresho ya miundombinu ya kidijitali, ambayo imeongeza ufanisi na ubunifu katika utoaji huduma.

Nsekela alisisitiza ukuaji wa benki umetokana na mikakati madhubuti, hali ambayo imefanya benki hiyo kuwa chaguo la kwanza kwa Watanzania.

"Tuzo hizi hazioneshi tu dhamira yetu ya kuwa benki kinara katika utoaji huduma bora na zinazokidhi mahitaji halisi ya wateja, bali pia zinaonesha namna gani tumekuwa tunasikiliza na kufanyika kazi maoni ya wateja na washirika wetu na jinsi ambavyo wafanyakazi wanajitoa katika kutoa huduma bora.

"Ni heshima kubwa kuwa Benki Salama na Benki Bora Tanzania, tuzo hizi zinatupa nguvu ya kusonga mbele katika kuwawezesha Watanzania na kuimarisha nafasi yetu kimataifa," Nsekela alisema.

Ikiwa na rasilimali za zaidi ya Sh. trilioni 14, Benki ya CRDB inashikilia nafasi kama benki kubwa zaidi Tanzania, inayotambulika kwa mafanikio endelevu katika viashiria vyote vya kiutendaji vya biashara.

Joseph Giarraputo, Mwanzilishi na Mhariri Mkuu wa Global Finance, alisema tuzo hizo pia zinatambua jitihada za Benki ya CRDB katika kukuza ujumuishi wa kifedha na kujenga imani ya wateja na wawekezaji, akisema:

"Katika mwaka uliopita, Benki ya CRDB imepiga hatua kubwa katika kutoa huduma bora na kujenga imani miongoni mwa wateja na wawekezaji ndani na nje ya nchi."

Wakati wa Mkutano Mkuu wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) jijini Washington D.C, Nsekela alishiriki pia kwenye mjadala maalumu kuhusu mifumo ya malipo kidijitali, akisisitiza dhamira ya Benki ya CRDB katika kukuza suluhisho za kidijitali zinazoboresha upatikanaji huduma za kifedha.

Nsekela pia alishiriki vikao vya kimkakati na taasisi za kimataifa kama vile WB, Benki ya Exim Marekani, MUFG, Yaatra Ventures na TIAA, Mfuko wa Pensheni wa Marekani unaolenga uwekezaji wa kimkakati barani Afrika, akilenga kufungua njia mpya za mitaji na kuiweka Tanzania kama kiungo muhimu kwenye uchumi wa dunia.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akipokea tuzo ya 'Benki Bora Tanzania' kutoka kwa Joseph Giarraputo, Mwanzilishi na Mhariri Mkuu wa Global Finance, katika hafla iliyofanyika Washington D.C. tarehe 26 Oktoba 2024. Katika hafla hii, iliyofanyika sambamba na Mikutano ya Mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, Benki ya CRDB pia ilitunukiwa tuzo ya 'Benki Salama.' **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Waziri awaomba viongozi wa dini wasaidie kukabili kipindupindu, Mpox

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Wizara ya Afya, Hassan Khamis Hafedh ameonya kuwa Serikali ya Zanzibar itawachukulia hatua kali madaktari na watendaji wa vituo vya afya wanaodharau na kutoa lugha za kejeli kwa wagonjwa.

Hafedh alitoa onyo hilo wakati akifungua mkutano wa kikao kazi cha kuongeza ufanisi wa uwajibikaji kwa madaktari na wasimamizi hao visiwani hapa.

Alisema hatua hiyo imekuja kutokana na wananchi kuwalalamikia madaktari juu ya utendaji wao wa kazi wakati wanakwenda kupata huduma za afya kwenye vituo hivyo na hospitalini.

Alisema baadhi ya madaktari wanapokuwa katika hospitali za serikali na kituo cha afya hawawajibiki ipasavyo, katika hospitali binafsi wakuwa karibu na wagonjwa kwa vile wanalipwa fedha nyingi.

"Tunafahamu kuwa baadhi yenu mkiwa katika hospitali binafsi mnakuwa na heshima kwa wateja wenu ila kwa serikali mnadharu haipendezi, " alisema Hafedh.

Alisema serikali ikitumia fedha nyingi kwa ujenzi wa hospitali na vituo vya afya, hivyo ni wajibu kwa watendaji hao kufanya kazi kwa kufuata madili na misingi.

Alisema Zanzibar ni nchi ya kitalii imekuwa na wageni wengi mchanganyiko, suala la afya ni muhimu, hivyo kuna kila sababu ya watendaji wa sekta hiyo kujipanga kuhimiza usafi.

"Kisiwa hiki ni cha utalii watu mbalimbali wanakuja kutembelea hapa hivyo watalamu wa afya wanatakiwa kufanya kazi zao za kuelimisha usafi na huduma bora wanazotoa," alisema Hafidh.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Mngereza Mzee Miraji, alisema kikao hicho kina lengo la kukumbushana juu ya utendaji kazi kwa madaktari na wasimamizi wa vituo vya afya vya Unguja.

Miraji, alisema kuna malalamiko kutoka kwa wananchi ya utovu wa nidhamu kwa baadhi ya madaktari na watendaji, hivyo wizara imejipanga kuwachukulia hatua kali.

"Kila mtu anafahamu kuwa kuna malalamiko mengi kwa baadhi ya watendaji wa afya kuwadharau na kuwatolea maneno ya kejeli wagonjwa, jambo hili halikubaliki," alisisitiza.

Wajumbe wa kikao hicho, walisema kikao hicho kinaenda kuamsha ari ya utendaji kwa madaktari wa Zanzibar kutokana na umuhimu wao mkubwa kwa jamii.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF iamke sasa, makosa ya kibinadamu yataishusha ligi

**KILA** msimu kunakuwa na makosa ya baadhi ya waamuzi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kwa namna walivyoanza msimu huu kuna uwezekano mkubwa ukatia fora.

Hata nusu msimu bado, lakini kumekuwa na malalamiko lukuki ya maamuzi ya hovyo, kwa baadhi ya waamuzi ambayo bila kupepesa macho 'yanaunajisi' mpira wa Tanzania.

Kuna kile kinachoelezwa kuwa makosa yanayofanywa na baadhi ya waamuzi ni ya kibinadamu, lakini ukiangalia kwa jicho la tatu unaweza ukapinga kuwa si ya kibinadamu kama inavyoelezwa kwani ni makusudi.

Bila kuitaja timu yoyote, lakini mara nyingi utakuta ni timu hiyo hiyo au hizo hizo ndizo zinazonufaika zaidi na makosa yao ya kibinadamu kupitia kwa waamuzi.

Tunavyotambua maana halisi ya makosa ya kibinadamu katika soka ni yale ambayo mwamuzi ni vigumu kuyabaini kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutokea kwa haraka zaidi kutokana na kasi ya mpira, lakini pia kila mmoja kuwa na mapungufu yake kama mwanadamu.

Lakini ukiona kila siku waamuzi hao hao wanafanya makosa yale yale kwa timu hiyo ama hizo hizo, basi dhana ya makosa ya kibinadamu hapo haipo, zaidi ya kusema kuna timu haitendewi haki na nyingine kubebwa.

Tulitegemea kama ni makosa ya kibinadamu, basi hata timu ambazo zinanufaika na zenyewe itokee siku ziathirike na makosa hayo hayo, yaani karibuni timu zote zifaidike dhidi yao, hayo ndiyo makosa ya kibinadamu tuyajuayo Nipashe.

Lakini makosa ya baadhi ya waamuzi wa Tanzania siku zote yanainufaisha timu moja zaidi au chache, hizo ndizo kila siku zinapata faida ya makosa hayo na zingine kazi yao ni kulia tu kwa kuonewa, hapo ni kuzifinyanga Sheria 17 za Soka.

Hapa ndipo wasiwasi wetu unapoanza kuja hasa kutokana na kauli baadhi ya mashabiki wanaposema bingwa wa msimu huu tayari ameshaandaliwa, ingawa hatutaki kuamini hivyo.

Lakini kingine kinacholeta wasiwasi ni waamuzi wanaoharibu ama kwa lugha yao, wenye makosa ya kibinadamu ni wale wenye majina makubwa na wazoefu wa kuchezesha mechi kubwa kubwa tu. Ukitazama katika michezo ya Ligi Kuu, kuna waamuzi wengi wapya, wanaume pamoja na kinadada ambao ni chipukizi, lakini wamekuwa wakichezesha vizuri michezo yao tofauti na hao wanaotajwa ni wazoefu.

Cha ajabu waamuzi wanaotegemewa ambao ni wazoefu, ukimuondoka, Ahmed Arajiga, wamekuwa wakifanya makosa mengi kwenye uchezeshaji wao kiasi cha mashabiki kujiuliza maswali mengi. Inawezekana hivi karibuni Kamati ya Bodi ya Ligi ambayo zamani ilifahamika kama Kamati ya Saa 72, ikakaa kwa ajili ya kupitia mwenendo wa michezo yote, lakini hilo lilipaswa kufanywa mapema zaidi, ili kuwa fundisho kwa wanaopewa nafasi ya kuchezesha mechi zinazofuata.

Tunachotaka sasa TFF na Bodi ya Ligi itoe adhabu kali kwa waamuzi wote ambao wameonekana kufanya makosa ambayo hayastahili hata kuwa na Video ya Usaidizi, VAR, ili kuyang'amua.

Tunatoa msisitizo huo kwa kuwa tuendapo tunaona sasa utafika wakati hata mashabiki wachache wanaojitokeza viwanjani wataona hakuna haja tena ya kwenda kwani tayari timu itakayoshinda inajulikana.

Hii itakuwa ni hasara kwa kila mtu, kuanzia TFF yenyewe, Bodi ya Ligi, klabu, wadhamini wa klabu na hata waliowekeza kwenye kurusha matangazo.

Sisi tunasikitika kuona klabu zikiwa zimewekeza kununua wachezaji wazuri na ghali kutoka nchi mbalimbali na kuifanya ligi yetu kuvutia, baadhi ya waamuzi wao wako kazini kushusha kiwango cha soka na kutaka kuturejesha kule kule tulipotoka kwa kutofahamu au kwa maslahi yao binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuna udhaifu wa wapiga faulo kwenye soka letu

Na Adam Fungamwango

**INAONEKANA** kuna matatizo ya 'maspesholisti' wa kupiga mipira iliyokufa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na soka la nchi hii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa takwimu za Kitengo cha Dawati la Michezo la Nipashe, kati ya mabao 135, yaliyofungwa mpaka leo hii kwa msimu huu, ni sita tu yamefungwa kwa mipira ya faulo za moja kwa moja.

Kwa maoni yangu, ni kiwango kidogo mno kwa idadi ya mabao ambayo yamefungwa mpaka sasa.

Takwimu zinaonesha kuwa winga wa Fountain Gate, Dickson Ambundo, ndiye anayeongoza akiwa amefunga mawili, Clatous Chama wa Yanga, Redemtus Mussa wa KMC, Ezekia Mwashilindi wa Prisons, Said Ndemla wa JKT Tanzania wote wamefunga bao moja moja.

Kwa Ligi Kuu kama ya Tanzania kuwa na idadi hiyo ya mabao ya mipira iliyokufa, inaonesha kuna matatizo sehemu ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi.

Inawezekana kwa miaka ya hivi karibuni hakuna wachezaji wenye vipaji vya kupiga mipira ya faulo kama ilivyokuwa zamani.

Nikirejea miaka ya nyuma kuanzia 1980 hadi 1990, kulikuwa na wachezaji waliokuwa na uwezo mkubwa wa kupiga faulo zilizokuwa hatari na mara nyingi zikizaa mabao.

Fred Felix Minziro wa Yanga alikuwa mmoja wa wachezaji wenye uwezo huo, kiasi cha staili yake ya upigaji kupachikwa jina la 'banana chop' kwani ilikuwa ni hatari sana, mpira ulikuwa unazunguka na kupinda kama ilivyo ndizi, hata kama akikosa, lakini kizaazaa lazima kiwapo langoni.

Wengine ni Ahmed Amasha wa Yanga, upande wa Simba alikuwa ni George Lucas, Hussein Masha na hata timu za mikoani zilikuwa na wachezaji ambao walikuwa ni maalum kwa mipira hiyo.

Na siyo faulo tu, hata kona pia kulikuwa na watu maalum, ambao zilipokuwa zinapigwa na kuzaa hatari sana langoni mwa timu pinzani.

Inawezekana pia wachezaji wa kisasa ni wavivu kufanya mazoezi ya kupiga faulo tofauti ya wale za zamani na hata nje ya nchi.

Tunaona baadhi ya wachezaji kwenye ligi za nje, wakifanya mazoezi ya faulo kwa saa nyingi kiasi kwamba timu yake ikipata faulo, si kama anakwenda kujaribu, bali kukifanyia kazi kile achokifanyia mazoezi.

Inawezekana pia ikawa walimu wengi na makipa wameshajua mbinu za wapigaji, hivyo kuweza kujipanga vema na kutoleta hatari.

Pamoja na yote hayo, ikumbukwe kuwa faulo ni moja kati ya njia ya kupata mabao kirahisi kwenye mchezo wa mpira wa miguu, kama timu itakuwa na mpigaji mzuri au wachezaji kujifunza namna ya kuwahadaa wapinzani wakati wa kupiga.

Mimi naona kama wachezaji wengi hufanya mzaha sana linapokuwa suala la kupiga faulo, lakini ni moja kati ya nafasi nzuri mno za kupachika mabao.

Inawezekana timu ikashindwa kupata nafasi dakika 90 za mchezo, lakini ikapata faulo hata nne ambazo zikitumiwa vema zinaweza zikazaa bao moja au mawili yanayoweza kuamua mechi.

Miaka ya katikati ya 1990, Simba ilipokuwa ikifundishwa na Dragan Popadic aliyekuwa raia wa Yugoslavia kwa wakati huo, sasa Serbia, aliweza kuifanya timu hiyo kuwa hatari mno kwenye mipira iliyokufa na kona.

Simba ilitwaa ubingwa mwaka huo na mabao yao mengi yalikuwa yakifungwa kwa kona na faulo, kiasi cha kuwatisha mpaka wapinzani kucheza rafu karibu na eneo la hatari na pia kuhofia kutoa kona.

Kocha huyo alikuwa na mafunzo maalum ya mipira iliyokufa na kona, akitumia mpaka ringi la basikeli kufunga pembeni juu ya lango na kuwataka wachezaji wapige faulo kupitisha katikati ya mzunguko wa ringi. Hii iliifanya timu iwe ya kutisha na iliweza kupata mabao kwa njia yoyote waliyoihitaji.

Kwa sasa, pamoja na kuonekana kupungua kwa vipaji na uvivu wa wachezaji, lakini pia hata mafunzo ya mipira iliyokufa kutoka kwa walimu imekuwa finyu. Wanatumia wale ambao angalau wanaonekana wana uwezo tu wa kupiga faulo na kuweza kulenga lango waamue. Nchini Afrika Kusini kwa sasa Klabu ya Mamelodi Sundowns, imeajiri makocha wa kufundisha kupiga faulo na pia kuzuia kufungwa aina hiyo ya mipira.

Nadhani hata hapa nchini kwa sasa wanahitajika, kama si kwenye klabu, basi hata Shirikisho la Soka nchini (TFF), liwaajiri kwa ajili kufundisha vijana wanaochipukia kwenye kituo chake cha malezi, ili baadaye nchi irejee kuwa na wapiga faulo wa kuaminika kama zamani.




Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile (kushoto), akimkabidhi tuzo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Nahodha Mussa Mandia (wa pili kulia). TASAC imetunukiwa tuzo hiyo kutambua mchango wake katika maendeleo ya sekta ya uchukuzi nchini. Tuzo hizo zilitolewa ikiwa ni sehemu ya Mkutano wa 17 wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi (JSTR), uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAC yajivunia kuvuka malengo yake kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limefanikiwa kufikia malengo yake yaliyowekwa katika mwaka wa fedha 2023/24 kupitia Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), kulinganishwa na miaka miwili iliyopita (2022/23 na 2021/22).

Nelson Mlali, aliyasema hayo alipotoa mada kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, wakati wa Mkutano wa 17 wa Tathmini ya Utendaji wa Sekta ya Uchukuzi (JSTR), uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), jijini Arusha.

Mlali ambaye ni Mkurugenzi Huduma za Biashara za Meli alisema ili kutimiza lengo lake la usimamizi na udhibiti wa-toa huduma katika sekta ya usafiri majini kama vile bandari za bahari Tanzania Bara, katika mwaka wa fedha 2023/24, TASAC imeweza kufuatilia vituo vyote vya bandari 60 vilizolengwa pamoja na bandari zote nane zilizolengwa kwa mujibu wa matakwa ya kimataifa ya Usalama wa Meli na Bandari (ISPS).

"Katika mwaka wa fedha 2023/24, tulifanikiwa kuvuka malengo ya utoaji vyeti kwa mabaharia 15,298 ambapo malengo yetu yalikuwa kutoa vyeti 10,000 kwa mujibu wa mkataba wa kimataifa (STCW standards)," alisema.

Mlali aliongeza kuwa shirika limeendelea kudhibiti ajali za baharini kwa vyombo vilivyo chini na zaidi ya tani ya jumla (GT) 50.

Katika kipindi cha ukaguzi, alisema shirika lilifikia malengo yake ya kutokuwa na ajali kwa vyombo zaidi ya tani ya jumla (GT) 50 pamoja na chini ya ajali tisa kwa vyombo chini ya tani ya jumla (GT) 50.

Alisema TASAC ililenga kupunguza muda uliotumika katika utoaji leseni kwa watoa huduma waliosimamiwa (ikiwa ni pamoja na waendeshaji wa bandari, waendeshaji wa bandari kavu, wakala wa meli na wakala wa ugomboaji shehena), ambapo wastani wa asilimia 94 ya waombaji walipewa leseni ndani ya muda uliowekwa.

"Mafanikio mengine ni matumizi ya mifumo katika utoaji huduma kwa wadau mbalimbali, ambapo mifumo miwili ilitengenezwa ambayo ni Mfumo wa Kusimamia Mapato TASAC (TASAC Revenue Gateway System - TRG) na Mfumo wa Utambuzi wa Mabahari," alisema.

Kwa mujibu wa Mlali, TASAC itaendelea kutekeleza majukumu yake ya udhibiti kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi, huku ikizingatia mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika sekta ya usafirishaji majini.

"Juhudi hizi za ushirikiano zitaongeza mchango wa usafiri wa baharini kwa uchumi wa taifa," alisema.

TASAC imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, ikiwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti sekta ya usafiri wa majini, kuwezesha biashara ya usafirishaji majini na kufanya biashara ya uwakala wa meli.

## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi ambao orodha yao ipo hapa chini waliolipia viwanja kwa nyakati tofauti eneo la Kikombo Kitalu "DA" na "N" kupitia benki, ila taarifa zao zinamapungufu ya majina, namba ya kiwanja na kitalu wafike ya Halmashauri iliyopo Manispaa ya zamani sehemu ya **mauzo ya viwanja** kwa ajili ya kuhakiki taarifa zao.

Muda wa utekelezaji ni kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2024 hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

Kushindwa kufanya hivyo, umiliki huo hautatambulika tena.

**ORODHA YA MAJINA YENYE TAARIFA PUNGUFU**

| NA | JINA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Christopher Kasung | 10,000.00 |
| 2. | Mbaga Iyombe | 1,000,000.00 |
| 3. | Veisi Maineko | 42,000.00 |
| 4. | George Abel Ngab | 300,000.00 |
| 5. | Ngalawe Hassan Ramadha | 6,931,641.00 |
| 6. | Esther Mpangala | 5,000,000.00 |
| 7. | Victoria Mgala | 400,000.00 |
| 8. | Godfrey K. Msongwe | 9,096,340.00 |
| 9. | Eliaza Mangera Wangwe | 5,148,000.00 |
| 10. | Florence N. Kebwe | 2,515,000.00 |
| 11. | Ali Hussein Habib | 338,300.00 |
| 12. | Joseph Lukumbika | 265,000.00 |
| 13. | Rosina J Delima | 2,249,554.00 |
| 14. | Kelvin Mlambalamba | 1,200,000.00 |
| 15. | Starphod Marwa | 1,000,000.00 |
| 16. | Ally H. Thabit | 3,000,000.00 |
| 17. | Mariam Tawakel | 10,000.00 |
| 18. | Jeremia Baha | 255,000.00 |
| 19. | Shani Mwaruka | 400,000.00 |
| 20. | Ramadhan N Simba | 50,000.00 |
| 21. | Ally Habiba Thabit | 3,000,000.00 |
| 22. | Job Ndalo | 100,000.00 |
| 23. | Giligoli A Ndaro | 100,000.00 |
| 24. | Gloria Reuben Ndaro | 80,000.00 |
| 25. | Magreth W Luma | 10,000.00 |
| 26. | Chedi Ng'enda | 21,729,382.00 |
| 27. | Sospeter N Marco | 2,500,000.00 |
| 28. | Geophrey Mtweve | 1,150,000.00 |
| 29. | Leonary Kimario | 24,000.00 |
| 30. | Lilian Sebastian | 1,625,000.00 |
| 31. | Anna Elisamehe | 400,000.00 |
| 32. | Olais Peter | 300,000.00 |
| 33. | Mussa Deogratius Limb | 4,566,560.00 |
| 34. | Marium | 225,000.00 |
| 35. | Rainer | 4,607,934.00 |
| 36. | George | 100,000.00 |
| 37. | Jafari | 500,000.00 |
| 38. | Dann | 10,000.00 |
| 39. | Victoria | 1,015,000.00 |
| 40. | Jona | 50,000.00 |
| 41. | Alvin | 677,100.00 |
| 423. | Christina | 700,000.00 |
| 43. | Tina | 100,000.00 |
| 44. | Doreen | 300,000.00 |
| 45. | Kelvin | 1,500,000.00 |
| 46. | Innocent | 1,000,000.00 |
| 47. | Mabrouk | 100,000.00 |
| 48. | SHM | 1,000,000.00 |
| 49. | Khadija | 500,000.00 |
| 50. | Jackline | 40,000.00 |
| 51. | Zubeda | 100,000.00 |
| 52. | Kelvin | 250,000.00 |
| 53. | Antony | 180,000.00 |
| 54. | Stanley | 3,500,000.00 |
| 55. | Kelvin | 250,000.00 |
| 56. | | 2,000,000.00 |
| 57 | | 220,000.00 |
| 58. | | 4,447,406.00 |
| 59. | | 2,000,000.00 |
| 60. | | 5,000,000.00 |
| 61. | | 1,566,355.00 |

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

# Anglikana kuadhimisha miaka 100 kifo cha mwasisi wa VETA

**Na Steven William,**
MUHEZA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Tanga, limeandaa maadhimisho ya miaka 100 tangu kifo cha mwasisi wa Chama cha Skauti na Mfumo wa Mafunzo ya Elimu ya uUfundi Stadi (VETA) nchini, Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Zanzibar na Tanga, Frank Weston.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania na Dayosisi ya Tanga, Maimbo Mndolwa, alisema kuwa Novemba 17, mwaka huu, kanisa litafanya kilele hicho cha maadhimisho hayo katika Kanisa la Msalaba Mtakatifu Magila, wilayani Muheza, mahali alikozikwa Askofu Weston mwaka 1924.

Akitoa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari nje ya Kanisa la Msalaba Mtakatifu Magila, Askofu Mndolwa alisema maadhimisho hayo yatatanguliwa na matembezi ya njia ya msalaba kuanzia msitu wa Nilo Novemba 6 hadi Novemba 17, siku ya kuhitimisha huko Magila Msalabani.

"Tunamwadhimisha Askofu Frank Weston, kwa kuwa ndiye mwanzilishi wa Chama cha Skauti Tanzania, chombo ambacho aliona vyema kifanye kazi ya kuwaimarisha vijana ambao walikuwa goigoi alipokuwa akiongozana nao katika safari wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia.

"Askofu Frank pia ndiye mwanzilishi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi hapa Tanzania, kupitia shule yetu kule kiwandani. Haya ni machache kati ya mengi ambayo Askofu Weston aliyafanya kwa afya ya kanisa na taifa letu la Tanzania," aliongeza Askofu Mndolwa.

Alisema ibada ya maadhimisho hayo Novemba 17, mwaka huu, itahudhuriwa na wageni kutoka nchi za Marekani, Uingereza, Zambia na Dayosisi za Kanisa Anglikana Tanzania ambazo Askofu Weston alipita huko na kufanya kazi ya injili.

Askofu Weston, alizaliwa Septemba 13, 1871 huko London, Uingereza na kufariki dunia Novemba 2, 1924 katika nyumba ya uaskofu iliyokuwa kilima cha Hegongo huko Magila Msalabani, wilayani Muheza.

# Hakimu abana upande wa mashtaka, ndugu wataka Jaji Mkuu aingilie kati

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imeutaka upande wa mashtaka katika kesi ya uhujumu uchumi, inayomkabili mfanyabiashara na mwekezaji Saleh Salim Alamry (54) na mwenzake Wakili Sheck Mfinanga, kuharakisha upelelezi wa shauri hilo, ili kesi ya msingi ianze kusikilizwa.

Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Erasto Philly, alielekeza hayo baada ya Wakili wa Upande wa Mashtaka, Ahmed Mbagwa, kudai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika ikiwa ni mara ya tatu kutoa taarifa ya aina hiyo mahakamani, kila washtakiwa wanapofikishwa mbele ya mahakama hiyo.

"Shauri limekuja kwa ajili ya kutajwa, kwa sababu upelelezi haujakamilika ila umefikia hatua nzuri, tunaomba ahirisho wakati upelelezi ukiendelea," alidai.

Mawakili wa Utetezi wa mfanyabiashara huyo, wakiongozwa na Moses Mahuna na Faisal Rukaka, walipinga maelezo ya Wakili Mbagwa na kueleza mahakama kuwa mteja wao anateseka na mahakama inatumika kama kichaka cha kumtesa.

"Haiwezekeni kila mara upelelezi haujakamilika na mara ya mwisho upande wa mashtaka hawakufika mahakamani bila taarifa yoyote.

"Ni bora waondoe kesi mahakamani na kumkamata tena na kumfikisha polisi kuliko kila mara kudai upelelezi haujakamilika," alidai Wakili Mahuna.

Alidai kwamba hakuna haja kumkamata mteja wake na kumfikisha mahakamani na kumpa kesi ya uhujumu uchumi wakati wanajua hawana uhakika na mashtaka yao. "Unawezaje kumkamata mtu na kumpa makosa ya uhujumu uchumi? Unajuaje kama alitenda kosa hilo halafu unamfikisha mahakamani na kudai upelelezi hujakamilika?

"Hii inasikitisha na kutia aibu kwa maofisa wa serikali kuendelea na shauri bila kuwa na uhakika na makosa ya mshtakiwa na mahakama wanaitumia kama kichaka cha kumtesa mteja wetu.

"Ninaomba mahakama itoe amri ya kuwataka upande wa serikali kukamilisha upelelezi au waondoe mashtaka na wamkamate hapo nje, ili wamfikishe polisi wakaanze upya," aliwasilisha hoja yao.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Philly alisema kuwa, "wakati unapomleta mshtakiwa mahakama na kushindwa kumsikiliza kwa wakati ni kumnyima uhuru na haki yake".

Alisema mahakama hiyo inasisitiza upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka, ili kesi hiyo ianze kusikilizwa.

Hakimu Philly aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 7, mwaka huu na kuzitaka pande zote kufika kwa wakati mahakamani na mshtakiwa Saleh alirudishwa mahabusu gerezani na mshtakiwa wa pili Sheck Mfinanga anaendelea na dhamana yake .

Nje ya mahakama, mmoja ya ndugu wa mshtakiwa, Asma Salimu, alimwomba Jaji Mkuu kuingilia kati shauri hilo, ili mshtakiwa ambaye ni kaka yake, apate haki yake ya msingi, akidai kesi hiyo "ni ya kupikwa kwa lengo la kumshurutisha', ili ajitoe kwenye kampuni kadhaa anazomiliki baada ya kutokea mgogoro wa kibiashara na wawekezaji wenzake ambao wako Saud Arabia.

Asma alidai ndugu wanashangazwa na mahakama kudai haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo wala kutoa amri zozote pasi na kupata hati au rukhsa ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali, ilhali mahakama hiyohiyo imetoa dhamana kwa mshtakiwa namba mbili ambaye pia anakabiliwa na shtaka hilo la uhujumu uchumi. "Kama mshtakiwa namba mbili ameachiwa na hakimu, basi na ndugu yetu aachiwe kwa dhamana maana wote wanatuhumiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi, ambayo kisheria hayana dhamana.




Meneja wa Bank of Africa Tanzania (BOA) tawi la Mbeya, Agatha Lyimo (katikati), akielezea huduma za benki hiyo, kwa wageni waliotembelea banda la maonesho la benki wakati wa Maadhimisho ya Nne ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yajizatiti kuwezesha kampuni za Korea zinazotekeleza miradi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesisitiza kuendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwezesha kampuni kutoka Korea Kusini zenye nia ya kuwekeza nchini, ikiwa ni sehemu ya jitihada zake za kuchangia ukuaji uchumi endelevu.

Mkuu wa Kitengo cha Miamala wa benki hiyo, Linda Teggisa, alisema hayo wakati ya semina ya '2024 Korea - Tanzania Project Plaza' iliyofadhiliwa na Benki ya NMB na kukutanisha zaidi ya kampuni 100 jijini Dar es Salaam na mtandaon, jana.

"Dhamira yetu iliimarishwa zaidi baada ya kutia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Shirika la Korea Kusini, linalojihusisha na kufadhili miradi katika sekta ya ujenzi la Korea Finance for Construction (K-FINCO) miezi michache iliyopita. Kupitia ushirikiano huu, tunalenga kupanua masuluhisho yetu ya kifedha zaidi kwa kupitia ufadhili wa vifaa, ili kusaidia utekelezaji miradi.

"Tunatarajia kupanua wigo wetu kwa kutoa huduma zingine ikiwa ni pamoja na kutoa ufadhili wa mitaji, ufadhili wa mali na masuluhisho ya miamala, ili kuongeza mnyororo mzima wa thamani wa miradi," alisema.

Alibainisha kuwa Benki ya NMB itaendelea kuwa mdau madhubuti katika ufadhili wa miradi ya kimkakati kupitia ubia na taasisi kubwa za fedha duniani, huku akipongeza serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara.

"Mfumo imara kwa kiasi kikubwa umechangia ukuaji sekta ya benki na fedha katika miaka ya hivi karibuni. Sekta ya benki imeshuhudia ukuaji mkubwa katika utoaji mikopo kutoka Sh. trilioni 34.6 mwaka 2021 hadi kufikia Sh. trilioni 46 kwa mujibu wa ripoti," alisema.

Alibainisha kuwa benki yake itaendelea kuchukua jukumu kuu katika kukuza ushirikishwaji kifedha kama sehemu ya juhudi za kuziba pengo kwa wasio na akaunti za benki.

Tegessia wakati wa hafla hiyo, alipongeza uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Korea Kusini na kuongeza kuwa, uhusiano kati ya nchi hizo mbili umeendelea kukuza maendeleo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, wakati wa hafla hiyo, alitoa rai kwa kampuni zaidi ya Korea Kusini kuja kuwekeza nchini.

"Kuna sababu lukuki za kwanini kampuni za Korea Kusini kuja kuwekeza Tanzania. Mbali na uhusiano wa muda mrefu wa nchi hizi mbili ambao nchi zote mbili zinaendelea kufurahia.

"Tanzania kwa miongo miwili iliyopita imeweka sera nzuri na thabiti za kiuchumi ambazo zimesababisha ukuaji wa wastani wa takriban asilimia saba kwa mwaka," alisema.

Teri alibainisha kuwa Tanzania ina fursa mbalimbali za uwekezaji, huku akisisitiza kuwa kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali, wawekezaji pia watanufaika moja kwa moja na jumuiya hizo.





## HABARI KASKAZINI



Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini, Shigeki Komatsubara (katikati), akikata utepe katika uzinduzi wa kaushio la zao la mwani katika hafla ya makabidhiano ya makaushio na mashine za kusaga zao hilo, jijini Dar es Salaam juzi, wa pili kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian na kulia kwake ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa Dk. Edwin Mhede, pia vifaa vya kuwawezesha wakulima wa mwani, na wafugaji wa jongoo bahari na kaa vilikabidhiwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# TANROADS kuanza ujenzi madaraja Arusha, K'njaro

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), unatarajia kuanza ujenzi wa madaraja ya juu, upanuzi wa barabara zinazoingia jijini hapa, ili kutoa huduma bora za usafiri kwa nchi za wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC).

Vilevile, utajenga madaraja mkoani Kilimanjaro eneo la Kibosho Shine na Mto Kikafu, ili kuimarisha usalama kwa watumiaji wa daraja hilo.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS nchini, Mohamed Best, alitangaza mpango huo, mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa.

Kwa mujibu wa Best, dhamira ya TANROADS ni kuhakikisha wanajenga barabara na madaraja ya juu na chini kwa kiwango chenye ubora.

Alisema kwa sasa wapo katika hatua za mwisho za usanifu wa kuanza ujenzi wa barabara kutoka Arusha-Tengeru, Tengeru-Athi River na kwenda Mkoa wa Kilimanjaro eneo la Kibosho Shine na daraja Kikafu.

"Tutaendelea kukuza ubora wa barabara katika majiji kwa kujenga madaraja ya juu, lakini kwa kupanua barabara kuu zinazoingia katika majiji makuu, ikiwamo Jiji la Arusha na hivi karibuni usanifu utakamilika," alisema.

**Alisema TANROADS wataendelea kufanya kazi kwa bidii kila siku, ili kuhakikisha miundombinu nchini inakuwa bora na kutoa fursa zaidi sio ndani ya nchi tu, hata nchi jirani ambazo zimeizunguka Tanzania.**

Best, alisema katika Mkoa wa Mwanza, watajenga barabara ya kutoka Usagara kwenda Kigongo Busisi na mkoani Dar es Salaam, barabara ya Ubungo kwenda Kimara, na tayari kazi inaendelea.

Kadhalika madaraja ya juu yanaendelea kujengwa mkoani Dar es Salaam kupitia ubalozi wa Japan na makutano ya Morocco na Mwenge.

Aliwaomba wananchi ambao ni wanufaika wa miundombinu ya madaraja na barabara hizo, kutunza kwa sababu ndio inayowaunganisha na ni kiungo cha usalama wa nchi.

Kwa upande wa wenye malori, aliwasihi kufuata viwango vya uzito wa magari yao, ili barabara zidumu kwa sababu zimejengwa zihudumie watu kwa kipindi cha miaka 15 hadi 16. "Hivyo muhimu wote tutunze na tusibomoe alama za barabarani na kuchukua vyuma vya madaraja, kwenda kufanya matumizi yasiyostahili," alisema Best.

Alisema TANROADS wataendelea kufanya kazi kwa bidii kila siku, ili kuhakikisha miundombinu nchini inakuwa bora na kutoa fursa zaidi sio ndani ya nchi tu, hata nchi jirani ambazo zimeizunguka Tanzania.

Alisema wataendelea kusimamia miradi mikubwa ambayo ni chachu ya maendeleo katika uchumi wa nchi.

# Pangani watakiwa kupanda mikoko pembeni mwa Bahari

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAKAZI wa Wilaya ya Pangani mkoani hapa wametakiwa kulinda na kutunza mazingira kwa kupanda miti ya mikoko pembezini mwa Bahari ya Hindi ili kuuacha hai ukanda wa Pwani na kuweka salama maisha yao.

Rai hiyo imetolewa wakati serikali imewekeza kiasi cha zaidi ya sh. bilioni 2 kwa ajili ya kujenga uzio pembezoni mwa bahari hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dkt. Ashatu Kijaji, alitoa rai hiyo katika Kijiji cha Masaika wilayani humo alipofanya ziara yake.

"Maji ni rasilimali ndipo tunapovua lakini ardhi yetu ni rasilimali ndipo tunapoishi, hatuwezi tukavua na kuishi baharini kama samaki hivyo ni lazima tuilinde nchi kavu yetu,

"Serikali yetu ni sikivu, imechukua hatua, lakini sio suluhisho la kudumu bali ni binadamu sisi kupunguza shughuli za kibinadamu ambazo zimeingia karibu na bahari, shughuli zetu za kiuchumi ni sawa, lakini msiingie kukata miti ya mikoko ili tuwe salama" alisema.

Akiwa wilayani Muheza, Dk. Kijaji alitembela kiwanda cha kuchakata mazao ya viungo cha GFP Organics L.T.D na kuwaeleza wafanyakazi kuwa serikali imeweka kipaumbele kwenye kilimo.

kwani Rais amepongeza bajeti ya sekta kilimo kutoka bilioni 200 mpaka kufikia zaidi ya sh trilioni 1.

Alisema bajeti hiyo imeongezeja zaidi ya asilimia 300 jambo ambalo linaonesha utayari wake wa kuwalea wakulima nchini ili kuinua kipato chao. "Taifa letu liko tayari kuimarisha kilimo chetu lakini huku tukitunza mazingira, bidhaa zetu zinazotengenezwa hapa zinakwenda nje ya nchi, ifahamike kuna Mataifa duniani yanahangaika kutafuta fedha za kigeni, hasa dola.

"Na sisi hapa tulipo tunaongelea Dola tuu na siyo fedha nyingine, Mh. Rais wetu yuko pamoja na ninyi, ataendelea kuiunga mkono sekta ya kilimo kwasababu inatengeneza ajira kwa vijana na wanawake.

Awali Meneja Usindikaji, Magreth Lutege kwa niaba ya Mkurugenzi wa GFP, alisema kilimo hai kina faida kubwa kwa mazingira, lakini bado wanakabiliana na matatizo kadhaa ukiwemo uelewa mdogo wa wadau kuhusu kilimo hicho.

Lutege, alisema imependekezwa utengwe ukanda wa kilimo hai ambao utapigwa marufuku matumizi ya kemikali hatarishi kwa mazao hayo na mazingira.

# Wakuu taasisi Wizara ya Uchukuzi wabanwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKUU wa taasisi za Wizara ya Uchukuzi na wenyeviti wa bodi wameagizwa kuhakikisha ujenzi wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao inakamilika kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Naibu Waziri wa wizara hiyo, David Kihenzile wakati akifunga mkutano wa 17 wa mapitio ya utendaji kazi na uchukuzi.

Kihenzile, alisema kuwa ametoa agizo hilo wakati serikali ikiwa mbioni kuanzisha kiwanda cha kutengeneza meli baada ya kukamilisha kutengeneza Meli ya Mv Victoria na kukarabati meli zilizopo.

"Sekta ya uchukuzi ndiyo sekta iliyopendelewa kuliko sekta yeyote nchini kwa kupewa fedha nyingi za kutekeleza miradi ili kuharakisha kasi ya maendeleo katika sekta hizo. Hivyo wakuu wa taasisi na wenyeviti wa bodi hakikisheni miradi yote inayotekelezwa katika maeneo yenu inakamilika kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa.

Alisema kutokana na umuhimu wa sekta hiyo, ufike wakati kwa kila taasisi kupima utekelezaji wa majukumu ya kila siku na kuweka mikakati kwa manufaa ya nchi.

Kuhusu sekta ya anga, Kihenzile, alisema serikali imetenga kiasi cha shilingi trilioni moja kuboresha viwanja vya ndege nchini na kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi sasa serikali imefanikiwa kununua ndege tisa zinazofanya safari za kimataifa na za kati.

Alisema Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri Ardhini (LATRA) imepiga hatua na kwamba hadi kufikia Disemba mwaka huu, mifumo yote itakuwa inasomana na wadau wa sekta binafsi wa mabasi baada ya kukamilisha mfumo wa utoaji tiketi.

Awali Katibu Mkuu Wizara hiyo, Profesa Godius Kahyarara, alisema Sekta ya Bandari nchini imepiga hatua kubwa na kwa sasa Bandari ya Dar es Salaam ina gati 13 na manufaa yake yameanza kuonekana.

Mwakilishi kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Mumina wa Kyendo, alisema mfumo wa usafiri ni muhimu sana kwa sababu unarahisisha uzalishaji mali.

"Naipongeza serikali ya Tanzania kwa kuwezesha sekta ya uchukuzi kwa sababu sekta ya uchukuzi ni mshipa ambao biashara hufanyika, na biashara haiwezi kufanyika kama hakuna uzalishaji, na uzalishaji hautakuwepo kama hakuna usafiri," alisema

Alisema anatarajia mwakani, wataona jinsi watakavyoshirikiana kusaidia mawazo na kufadhili chochote kinachohitajika kwenye miradi inayoendelea kujengwa.





# Dereva adakwa akiendesha basi kwa leseni ya pikipiki

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamshikilia dereva wa basi la abiria linalofanya safari kati ya Mwanza na Morogoro, kwa tuhuma za mwendo kasi na kukutwa na leseni ya kuendesha pikipiki kinyume cha sheria.

Dereva huyo alibambwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhani Ng'azi katika Kituo cha mabasi Tinde, mkoani Shinyanga, wakati wa ukaguzi wa mabasi yanayofanya safari usiku kutoka jijini Mwanza kuelekea mikoa mingine nchini.

**Katika opereshheni hiyo, mabasi 53 yalikaguliwa, kuandikiwa faini 15 na madereva waliobanika kutokidhi vigezo ni wawili.**

"Huyu sio dereva wa gari la abiria, leseni yake ukomo wake ni kuendesha pikipiki, hatuwezi kumvumilia kuendelea kufanya shughuli hii nyeti bila vigezo," alisema Ng'anzi.

Alisema wanaendelea na operesheni ya ukaguzi wa magari yanayofanya safari usiku kuanzia mkoani Mwanza na Shinyanga.

Katika operesheni hiyo, mabasi 53 yalikaguliwa, kuandikiwa faini 15 na madereva waliobanika kutokidhi vigezo ni wawili.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, madereva wa mabasi ya abiria 105 wamefungiwa leseni, baada ya kubainika kukiuka sheria za usalama barabarani, ikiwa ni ongezeko la madereva 10.

Alisema baadhi ya makosa hayo ni mwendo kasi, kuchezea mifumo ya udhibiti mwendo (VTS) na kuwa katika operesheni hiyo, mabasi mawili yamezuiwa kuendelea na safari kutokana na ubovu.

Ukaguzi huo unafanyika, ili kudhibiti ajali za barabarani zinazotokea hususani katika kipindi cha mwisho wa mwaka.



Kiongozi wa Timu ya Benki ya Dunia-WB (wa tatu kushoto), Prof. Roberta Malee, akizungumza na wataalam wanaotekeleza mradi wa ujenzi wa majengo ya Chuo cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kilichopo wilaya ya Butiama mkoani Mara, wakati wa ziara yake kutembelea taasisi za kielimu zilizonufaika na fedha za Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi Tanzania (HEET) Wengine katika picha ni viongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja watumishi wa chuo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 2bn/- kukarabati barabara korofi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mjini nchini (TARURA) wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga imeanza utekelezaji wa miradi ukatabati wa barabara yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.9.

Hayo yamebainishwa na Meneja wake, Mhandisi Joseph Mkwizu wakati akizungumza Nipashe kuhusu ujenzi wa barabara hizo ambazo zimekuwa zikikata mawasiliano hasa wakati wa mvua.

Mhandisi Mkwizu, alisema wameingia mikataba nane na wakandarasi ya matengenezo ya barabara hizo katika mwaka huu wa fedha wa 2024/25.

Alisema matengenezo hayo yatahusisha maeneo korofi ya kata za Majengo, Mhongolo na Mwime-Zongomela.

Alisema miradi mingine minne ambayo pia inaanza mwezi huu inatarajia kukamilika Februari, 2025 ikiambatana na uzibuaji mitaro ya maji na madaraja ili kudhibiti athari za mafuriko wakati wa mvua za masika.

"Tumewataka wakandarasi wote walioingia mikataba kuhakikisha wanawatumia vijana wa maeneo husika kwenye kazi ambazo hazihitaji ujuzi ili waweze kunufika na fedha hizo," alisema Mkwizu na kuonya kuwa:

" Wale watakaopata nafasi za kazi wasije kujihusisha kwenye vitendo vya wizi kwani watakwamisha matengenezo yasikamilke kwa wakati."

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi waliopo katika maeneo yenye miundombinu mibovu ya barabara, akiwemo Mkazi wa Mtaa wa Mwime Kata ya Zongomela, Daudi John, alisema eneo lao limekuwa na mafuriko mara kadhaa ikilinganishwa na maeneo mengine na wanafunzi kushindwa kwenda shule mpaka kipindi cha masika kinapomnalizika.

John, alisema ipo haja serikali kujenga mitaro imara kwenye barabara zote ili kudhibiti mafuriko kabla ya mvua kuanza kunyesha.

Martha Kosike, aliiomba TARURA baada ya kupata fedha za matengeenezo ya barabara, kuhakikisha mifereji iliyoziba kwa uchafu na madaraja inazibuliwa ili maji yapate sehemu ya kupita na kudhibiti mafuriko.

Dereva wa bajaj, Said Hamza, Mkazi wa Majengo, Said Hamza, alisema walichangisha fedha kwa kila kaya na kujenga mitaro baadhi ya maeneo korofi na kudhibiti maji kuingia kwenye makazi ya watu na kuwaomba TARURA kuwaunga mkono kwa kujenga mitaro maeneo mengine.

# Njiti, mama zao wapatiwa misaada

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATOTO zaidi ya 50 waliozaliwa kabla ya muda 'njiti' na mama zao waliolazwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure) wamepatiwa misaada ili kuwawezesha kukidhi mahitaji wakati wakipatiwa huduma.

Misaada hiyo ya vitu mbalimbali yakiwemo mafuta ya joto, maziwa, sabuni, daipazi na vifaa vingine vya usafi hospitalini vilitolewa juzi na wadau wa maendeleo kutoa Benki ya Baroda (T) Ltd, Tawi la Mwanza ikiwa ni maadhimisho ya Miaka 20 ya kuanza shughuli zake nchini.

Akikabidhi misaada hiyo, Meneja wa benki hiyo, Victoria Kavishe, alisema ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii kutokana na faida ambayo benki hiyo imepata na kuwakumbuka watu wenye uhitaji zaidi.

"Tumefikiishia miaka 20 toka tufungue benki yetu hapa Tanzania, hivyo tumeona ni jambo jema tusishereheke wenyewe bali kwa kuwagusa wenye uhitaji kwa kutoa kitu kidogo kwa mama wenye watoto waliozaliwa kabla ya muda wao," alisema Victoria.

Muuguzi wodi ya watoto wachanga katika hospital hiyo, Beatrice Kanja, alisema kwa siku inapokea watoto kuanzia 20 mpaka 50, ambao baadhi ya wazazi wao hawana uwezo wa kumudu mahitaji muhimu.

"Binafsi tunafarijika kuona wazazi na watoto wanapata mahitaji, hivyo tunawashukuru kwa misaada hii itakayowasaidia kinamama na kupunguza utegemezi kwa ndugu zao,"alisema Kanja.

Nipashe
# Spotika



MABAO 6 YA FAULO KATI YA 135 LIGI KUU UK. 14




# RAPHINHA ANAVYOSTAWI NA KUINOGESHA BARCA

**BARCELONA, Hispania**

MWANZONI mwa Julai, nahodha wa zamani wa Barcelona, Tente Sanchez, alizungumza kwa ajili ya mashabiki wengi alipowataka wababe hao wa Katalunya kumsajili nyota wa Hispania kwenye Euro 2024, Nico Williams.

"Kama kungekuwa na nafasi ya kumsajili, ningemsajili," alisema Sanchez akiiambia Sport.

"Kama kuna uwezekano, Raphinha anaweza kuondoka na tunaweza kupata fedha, ningemsajili Nico. Ninapotazama mechi na wote wawili wakicheza, mimi humzingatia zaidi Nico kuliko Raphinha."

Haya yalikuwa maoni ambayo si tu ya mashabiki, lakini wajumbe kadhaa wa bodi ya klabu, ambao waliripotiwa kutaka kumtoa Mbrazil huyo kwa klabu mbalimbali katika kipindi cha nje ya msimu na Raphinha hakuwa tayari kuondoka.

Mchezaji huyo sasa amethibitisha kwa dhati uamuzi wake wa kubaki na kuiongoza Barcelona kuanza kwa kampeni mpya.

Hat-trick yake dhidi ya Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ilikuwa hatua ya hivi karibuni zaidi ya mabadiliko ya Raphinha.

### Kuongeza kujiamini

Wakati magwiji wa zamani, mashabiki na wakurugenzi walimtilia shaka Raphinha, wachezaji wenzake na wanachama muhimu zaidi wa klabu walimwamini.

Kabla ya kampeni, kocha mpya, Hansi Flick, aliwaruhusu wachezaji kupigia kura kundi jipya la manahodha baada ya kuondoka kwa Sergi Roberto.

Raphinha alikuwa chaguo la kushtukiza kwa wale walio nje ya chumba cha kubadilishia nguo, lakini kitendo hicho kinachoonekana kuwa cha sherehe kimekuwa na mchango mkubwa.

"Kujiamini na imani ambayo kocha wangu na wachezaji wenzangu wameniweka ni muhimu sana kwangu," alifichua Raphinha kabla ya ziara ya Bayern Munich.

"Mawazo niliyoanza nayo msimu huu ni tofauti kulinganishwa na misimu iliyopita."

Takriban chochote kingekuwa uboreshaji katika ufunguzi wa Raphinha kwa kampeni ya 2023/24 ambayo alianza kwa kadi nyekundu dhidi ya Getafe, lakini wachache wameweza kufikia mlipuko wake wa msimu huu.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil, amekuwa mchezaji wa kwanza katika LaLiga kupachika mabao matano na asisti tano msimu huu, kiwango cha pande mbili cha matokeo ambacho ni wachezaji wengine watatu pekee katika ligi tano bora za Ulaya wanaweza kufikia.

### Uhuru wa nafasi

Wakati wa misimu miwili ya Raphinha akiwa Leeds United, asilimia 85 ya mechi zake za Ligi Kuu England alikuwa akicheza winga ya kulia.

Xavi Hernandez, kwa kiasi kikubwa alimbadilisha na kumweka upande wa kushoto kwenye ubavu wake hadi alipoinuka Lamine Yamal katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

"Pia nimeelewa kwamba ikiwa nilitaka kuchezea klabu hii, nilipaswa kuzoea nafasi tofauti," alisema Raphinha, baada ya kujipanga upande wa kushoto dhidi ya Bayern.

Flick bado hajamwanzisha Mbrazil huyo kwenye upande wa kulia, lakini anampa nahodha wake uhuru wa kuzurura katika nafasi tatu za mwisho.

Kurejea katika utimamu wa Alejandro Balde, ambaye hutoa upana kwenye ubavu wa kushoto kwa kushambulia kutoka kwa beki wa pembeni, kunamruhusu Raphinha kutangatanga hadi kwenye nafasi hatari zaidi za uwanja.

Mchezaji huyo namba 11 wa Barcelona, ana wastani wa kuguswa zaidi kwenye eneo la hatari msimu huu, kuliko wakati mwingine wowote katika maisha yake ya soka tangu ajiunge na Sporting CP mwaka 2018.

### Utambulisho wa kiwango

Flick amehamisha aina yake ya mpira wa miguu hadi Katalunya. Katika mechi dhidi ya Bayern, ambayo ilikuwa ya ukali vile vile.

Raphinha amestawi chini ya utambulisho huu wa nguvu. "Sijawahi kuwa na mchezaji kama Raphinha katika timu yangu yoyote," alisema Flick, baada ya mchezo.

"Anajitolea kwa kila kitu. Anaweka moyo wake ndani yake. Akiwa na bila mpira, ni mzuri sana, huwa anaanza kushinikiza, anamaliza nafasi zetu. Anatabasamu kila wakati."


Kicheko hicho kilionekana wazi baada ya sekunde 58 za mechi ya Jumatano na kwa shida hakuacha uso wake katika kipindi kizima cha shindano.

"Ni wakati wa kusahau yaliyopita na kufikiria zaidi juu ya sasa tuliyonayo," alisema Raphinha. "Nina furaha sana kuwa hapa."

Kila mtu anayehusishwa na Barcelona anafurahi sana kwamba alibaki.

## ISIKUPITE

KAMA Real Madrid isingekubali kichapo cha mabao 4-0 kwenye LaLiga kutoka kwa Barcelona katika Uwanja wa Bernabeu juzi usiku, ingefikia rekodi iliyowekwa na Barca ya kucheza mechi 43 kwenye ligi bila kupoteza, ambayo iliiweka kati ya Aprili 2017 na Mei 2018.



Extra Time




# KITENDAWILI CHA SALAH, VAN DIJK NA ALEXANDER-ARNOLD LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

WAKATI Arsenal ilipofungwa na Bournemouth na Manchester City kuendeleza ushindi mwingine bila Rodri ambaye ni majeruhi, Liverpool ilichapisha matokeo yao bora zaidi ya msimu huu kufikia sasa: ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chelsea, kwenye Uwanja wa Anfield.

Ushindi huo uliwarudisha kileleni mwa jedwali na kuwafanya kushinda mara saba kati ya mechi nane za ligi na 10 kati ya 11 katika mashindano yote chini ya kocha mpya, Arne Slot.

Pamoja na ushindi dhidi ya Chelsea, Slot amekuwa kocha wa pili kwa kushinda kwa haraka zaidi mechi 10 za Ligi Kuu nyuma ya Pep Guardiola pekee.

Na licha ya kuruhusu bao dhidi ya Chelsea, timu yake bado imeruhusu mabao matatu pekee msimu mzima au tano pungufu, kuliko timu nyingine yoyote.

Pamoja na hayo yote, muda mfupi unaonekana bora zaidi kuliko muda mrefu.

Wachezaji watatu bora wa Liverpool, Virgil van Dijk, Mohamed Salah na Trent Alexander-Arnold, wote wamebakiza chini ya mwaka mmoja kwenye mikataba yao.

Ingawa haiwezekani, klabu imeunda hali ambapo sasa kuna nafasi ya kweli kwamba timu hii itashinda Ligi Kuu au Ligi ya Mabingwa Ulaya - na kuwapoteza Van Dijk, Salah na Arnold bure.

Kuna ulimwengu mwingine, ingawa haiwezekani zaidi, ambapo wachezaji wote watatu wanakubali mkataba na timu mpya kabla ya msimu huu kumalizika.

Kufikia Januari Mosi, mwakani, wote wataweza kuingia kwenye mazungumzo na klabu mpya za nje na ndani ya England.

Kwa hiyo tulifikaje huko? Na ni matokeo gani yanayowezekana zaidi kwa hali ya sintofahamu inayoizunguka timu hiyo ambayo kwa sasa imeanza vema tangu mara ya mwisho (na ya kwanza) ilipotwaa ubingwa wa Ligi Kuu?

### Kwa nini Liverpool wako katika hali hii?

Baada ya Liverpool kukaribia kushinda kila taji mnamo 2022, lakini wakakosa ubingwa wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya, mambo mawili yalibadilika.

Si uwanjani, Michael Edwards alijiuzulu kutoka kuwa mkurugenzi wa jukumu la soka na wamiliki wa klabu, Fenway Sports Group walielezea uwezekano wa kuuza timu.

Kwa upande wa watendaji wenye matokeo katika Ligi Kuu ya kisasa, Edwards anaweza kuwa nambari moja.

Alijenga upya akademi ya klabu, akamwajiri Jurgen Klopp kuchukua nafasi ya Brendan Rodgers, na kuipa mamlaka idara ya utafiti ya klabu hiyo kuhusika katika ununuzi wote wa wachezaji na makocha.

Kwa maneno mengine, alisimamia kila kitu kilichosaidia Liverpool kurudisha hadhi yake ya kuwa moja ya timu bora zaidi ulimwenguni.

Katika miaka yao ya utukufu, maamuzi ya kuunda kikosi cha Liverpool hatimaye yalifanywa na mchanganyiko wa Edwards, Klopp na rais wa FSG, Mike Gordon, ambaye ndiye alikuwa daraja la mawasiliano ya walimu wa Liverpool na uwanjani.

Ilionekana kama mchakato huo ungeendelea bila Edwards, pia ilitangazwa kuwa anajiuzulu mwishoni mwa msimu mnamo Novemba 2021, kwa hiyo kulikuwa na wakati mwingi, na mwishowe, Mkurugenzi wa Ufundi wa Klabu, Julian Ward, aliteuliwa kama mbadala wake msimu wa majira ya joto wa 2022.

Lakini basi, miezi michache baadaye, mnamo Novemba 2022, Ward ghafla aliweka notisi yake; aliondoka kwenye klabu hiyo mwishoni mwa msimu. Vivyo hivyo kwa Ian Graham, mkuu wa idara ya utafiti.

Wakati haya yote yakitokea, habari ziliibuka kuwa FSG walikuwa wakijaribu kuiuza klabu hiyo.

Wakati huo huo, wachezaji ambao Liverpool walikuwa wameanza kuwanunua - Luis Diaz kutoka FC Porto, Darwin Nuñez kutoka Benfica, Cody Gakpo kutoka PSV - walianza kubadilika.

Hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa mchezaji mbaya, lakini hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa aina ya nyota wa uhakika au ununuzi wa bei nafuu wa hali ya juu na idadi nzuri ya msingi ambayo ilifadhili msingi wa timu.

Wote wawili Diaz na Nunez walikuwa hatua hatari, wakitokea Ligi ya Ureno - hasa Nunez, ambaye uhamisho wake uligharimu euro milioni 75, na alikuwa akitoka katika msimu wa majira ya joto usio na joto.

Gakpo, wakati huo huo, alisajiliwa mara tu baada ya kuibuka nyota kwenye Kombe la Dunia la 2022 akiwa na Uholanzi, mahali pa mwisho ambapo kwa kawaida timu yoyote inaweza kwenda kupata thamani katika soko la uhamisho.

Kitu ambacho watatu hao walikuwa nacho kwa pamoja ni tabia bora za kimaumbile - au kile unachoweza kutarajia wakati kocha ana ushawishi mkubwa katika upataji wachezaji.

Huku FSG ikilenga kuuza badala ya kuendelea na kikosi na bila Edwards klabuni tena, Klopp alionekana kuziba pengo la nguvu. Angalau, Ward na Graham waliondoka kwa sababu waliona kama kazi yao haikuwa na mchango tena.

Kisha, majira ya joto yaliyopita, klabu ilimwajiri Jorg Schmadtke - rafiki wa Klopp - kuwa mkurugenzi wake wa muda wa michezo kwa mwaka mmoja.

Na kisha Klopp mwenyewe akatangaza kuwa ataondoka katika klabu hiyo katikati ya msimu uliopita.

Baada ya kusoma yote hayo, pengine haitakushangaza kusikia kwamba klabu hiyo imemsajili tena mchezaji mmoja tu ambaye si wa akademi tangu Novemba 2022.

Na mchezaji huyo ni beki wa kushoto wa akiba, Kostas Tsimikas, ambaye ni mmoja wa wachezaji wa chini.

Tangu Edwards alipoondoka, kimsingi kumekuwa hakuna mtu wa karibu na uongozi wa klabu akiangalia hali ya mikataba ya muda mrefu ya wachezaji.

FSG walikuwa wakijaribu kutafuta mtu wa kuwalipa mabilioni ya dola ili kupata timu; Ward alijiondoa kwa miezi michache tu, Schmadtke aliajiriwa kwa muda tu.

Na Klopp? Kweli, hakujua jinsi ya kusimamia malipo ya klabu kubwa ya soka kwa sababu yeye ni mkufunzi wa soka. Zaidi ya hayo, alijua kwamba hakuwa na muda mrefu kwa klabu.

Si tu kwamba hakukuwa na mtu wa kuweka vipaumbele au hata kufanya maamuzi haya makubwa, kwa nini yeyote kati ya wachezaji hawa angeangalia hali hii, aone msukosuko wa kila mara kati ya watu wanaoamua mikataba yao.

FSG wamejitoa tena kwa klabu baada ya kushindwa kupata mnunuzi mkubwa; Edwards amerejea katika nafasi iliyo juu ya Mkurugenzi wa Michezo; Richard Hughes, aliletwa kutoka Bournemouth kutekeleza katika nafasi ya mkurugenzi wa michezo; Ward amerejea kama mkurugenzi wa ufundi. Na idara ya utafiti haijawekwa kando tena.

Lakini yote haya yaliimarishwa msimu huu wa kuchipua, pale wachezaji watatu nyota wa timu hiyo walipoingia miaka ya mwisho ya mikataba yao.

Kwa machafuko yote juu ya shughuli nyepesi ya Liverpool kwenye soko la usajili wa majira ya joto, kufikiria mustakabali wa Salah, Van Dijk, na Alexander-Arnold inapaswa kuwa.

### Salah, Van Dijk, na bei zao

Hali za Salah na Van Dijk zinavutia, kutoka kwa mtazamo wa kinadharia na soko.

Salah atakuwa na umri wa miaka 33 mwanzoni mwa msimu ujao; Van Dijk miaka 34.

Kwa upana, tunajua kwamba wachezaji wote wawili wanapaswa kuwa tayari wamepita kilele chao na wanaweza kuwa katika hatari ya kushuka kwa ghafla.

Hasa zaidi, ingawa, wote wawili bila shaka bado ni wachezaji wawili bora zaidi ulimwenguni katika nafasi zao. Wakati mchambuzi Bob Hayes alipofanya utafiti kuhusu kuzeeka katika soka, aligundua kuwa wachezaji walio na viwango vya juu vya ustadi wa kimwili na kiufundi walielekea kuzeeka zaidi.

Na wale wanaotegemea zaidi ujuzi wa kimwili wenye umri mbaya zaidi kuliko wale ambao walitoa thamani na uwezo wao wa kiufundi.

Salah na Van Dijk ni wazi wote wanalingana katika kitengo hicho cha kwanza cha nyota wa kimwili na kiufundi.

Ni kwamba hakuna ushahidi mwingi wa mabeki kucheza kiasi hicho kwenye Ligi Kuu kuanzia umri wa miaka 34 na kuendelea, na kuna ushahidi mdogo wa kucheza kwa kiwango cha juu.


SLOT, VAN DJIK, SALAH, TRENT

## Nukuu

"Simba ni kubwa kuliko mtu binafsi...si mara zote mchezaji bora uwanjani, ila timu bora zaidi uwanjani..." **Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Namungo FC, wiki iliyopita.**



"Ni wakati mgumu, wakati mgumu unapopoteza mchezo, hasa baada ya mechi nyingi bila kufungwa," **alisema Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, baada ya kichapo cha mabao 4-0 dhidi ya Barcelona, ambapo kama wangeshinda wangetimiza mechi 43 za ligi bila kupoteza.**



"Ninataka kwenda kwenye timu inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, baada ya kuondoka Fenerbahce, ili nisicheze katika mashindano ya Uefa," **Jose Mourinho, baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi ya Europa, wiki iliyopita.**





Winga wa Yanga, Maxi Nzengeli, akimbeba na kumpongeza, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama, baada ya kufunga bao kwa faulo ya moja kwa moja katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na JKT Tanzania, uliochezwa, Oktoba 22, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, likiwa ni bao la sita kufunga msimu huu, kwa njia hiyo mpaka kufikia raundi ya tisa. . **PICHA: MTANDAO**

# MABAO 6 YA FAULO KATI YA 135 LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HADI kufikia jana, jumla ya mabao 135 yamefungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo imeingia raundi ya tisa, huku baadhi ya timu zikiwa zimecheza michezo minane, Mashujaa FC na Yanga zikiwa zimecheza michezo zaidi, saba kila moja.

Kati ya mabao hayo, ni sita tu ndiyo yamefungwa kwa mikwaju ya faulo za moja kwa moja mpira ukatinga wavuni.

Timu ambazo mpaka sasa zimefanikiwa kufunga mabao ya faulo za moja kwa moja ni Fountain Gate ambayo imepachika mawili, Yanga, KMC, Prisons na JKT Tanzania.

Katika makala haya tunakuletea rekodi za faulo zote hizo, jinsi zilivyofungwa pamoja na wachezaji ambao wamezipachika nyavuni.

**1# Dickson Ambundo - (Fountain Gate vs Dodoma Jiji)**

Dickson Ambundo, winga wa zamani wa Yanga, ndiye mchezaji wa kwanza msimu huu kufunga bao la faulo ya moja kwa moja kwenye Ligi Kuu.

Alifanya hivyo Septemba 15 mwaka huu, wakati timu yake ya Fountain Gate ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa uliopo Babati, Karatu.

Ilitokea faulo kwenye wingi ya kushoto nje kidogo ya eneo la hatari la Dodoma Jiji, huku wachezaji wawili wakijipanga kupiga.

Alikuwa ni Ambundo na Amos Kadikilo. Wakati wote wakidhani Kadikilo atapiga na mguu wa kushoto, Ambundo alipiga faulo kwa mguu kulia uliokwenda kutinga kwenye engo ya pembeni juu ya lango la Dodoma Jiji.

Bao hilo lilifungwa dakika tano kabla ya mechi kumalizika na lilikuwa la kusawazisha, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

**2# Redemtus Mussa - (KMC vs KenGold)**

Siku moja baada ya kupatikana kwa bao la kwanza la faulo kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, katika Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, lilipatikana bao la pili lililowekwa wavuni na Redemtus Mussa, KMC ikicheza dhidi ya KenGold.

Ibrahim Elias aliangushwa nje ya eneo la hatari pembeni, wingi ya kulia na mwamuzi akaamuru faulo.

Ilionekana kama mpigaji atapiga krosi, kwa sababu faulo hiyo ilitokea karibu na kibendera cha kona.

Haikuwa hivyo, Redemtus alitumia mguu wake wa kushoto kupiga mpira huo kuelekea golini moja kwa moja, ukawachanganya beki na kipa wake kabla ya kujaa wavuni, dakika ya 14, mechi iliyochezwa Septemba 16, mwaka huu, KMC ikiondoka na ushindi wa bao 1-0.

**3# Ezekia Mwashilindi - (Prisons vs Fountain Gate)**

Beki wa Prisons, Ezekia Mwashilindi, anaingia kwenye rekodi ya kuwa mmoja wa wachezaji waliofunga mabao kwa faulo za moja kwa moja, kwenye Ligi Kuu msimu huu, baada ya kufanya hivyo, Oktoba Mosi, mwaka huu, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, timu yake ikicheza dhidi ya Fountain Gate na kuondoka na ushindi wa mabao 3-2.

Beki mmoja wa Fountain Gate aliunawa mpira nje na mbali kidogo ya eneo la hatari. Ilikuwa ni pembeni kidogo wingi ya kushoto.

Aliupiga kiufundi zaidi na kuonekana kama unatoka nje, lakini ulizunguka na kujaa wavuni, akiipatia timu yake bao la kusawazisha dakika ya 48.

Wakati huo timu yake ilikuwa nyuma kwa mabao 2-1 na kuingia kwa bao hilo kuliamsha ari ya wachezaji wenzake, dakika mbili baadaye wakapachika la tatu lililofungwa na Vedatus Mwihambi.

**4# Said Ndemla - (JKT Tanzania vs Tabora United)**

Kiungo mshambuliaji wa JKT Tanzania, Said Ndemla yumo kwenye orodha hii, baada ya kupiga faulo ya moja kwa moja iliyozaa bao la nne katika mchezo uliochezwa, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Oktoba 18, mwaka huu, dhidi ya Tabora United, ikishinda mabao 4-2.

Kipa raia wa Nigeria, Sochima Victor, alitokea na kuudaka mpira nje ya mstari, hivyo kusababisha faulo na yeye mwenyewe kuoneshwa kadi nyekundu.

Faulo iliyopigwa kwa shuti kali umbali ya mita yadi 35 hivi na kwenda moja kwa moja wavuni, dakika ya 68 ya mchezo.

**5# Dickson Ambundo - (Fountain Gate vs KMC)**

Kwa mara nyingine tena, Ambundo anarejea tena katika orodha na rekodi ya wapachikaji mabao ya faulo kwenye Ligi Kuu.

Safari hii akifanya hivyo, Oktoba 21, mwaka huu, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Manyara timu yake ikicheza dhidi ya KMC na kuibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Alipiga faulo mbali kiasi cha takriban yadi 30 hivi, bila yoyote kudhania kama lingeweza kuwa bao.

Lilikuwa ni shuti dhaifu, kwa mastaajabu wa wengi, kipa Fabian Mutombora raia ya Burundi, alionekana kama ameukamata, lakini ulimpita tobo na kujaa wavuni dakika ya nane ya mchezo.

Ndiye anaongoza kwa kufunga mabao mengi ya faulo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**6# Clatous Chama - (Yanga vs JKT Tanzania)**

Rekodi inaonesha kuwa, Clatous Chama ni mchezaji pekee wa kigeni aliyefunga bao la faulo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Watano waliobaki wote ni wazawa.

Chama alifunga bao kwa mtindo huo, Oktoba 22, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, akiisaidia timu yake kushinda mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania.

Makosa yalianzia kwa kipa Denis Richard, aliyedaka shuti la Pacome Zouzoua nje ya eneo analoruhusiwa kufanya hivyo.

Moja kwa moja alizawadiwa kadi nyekundu na timu yake kulazimika kumtoa Hassan Kapalata na kumuingiza kipa mwingine, Omary Gonzo, ambaye alishindwa kuzuia faulo ambayo alisababishwa na mwenzake, iliyopigwa na Chama.

**JE, WAJUA?**



USHINDI wa bao 1-0 Manchester City iliyoupata dhidi ya Southampton juzi, umeongeza rekodi yao ya kutopoteza kwenye Ligi Kuu hadi mechi 32. Sasa imebakiza wiki sita tu kumaliza miezi 12 tangu ilipopoteza ugenini kwa mara ya mwisho, dhidi ya Aston Villa Desemba 6, mwaka jana.





# Vijana watakiwa kuacha kusubiri ajira serikalini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za kilimo, ili kujipatia kipato badala ya kusubiri ajira kutoka serikalini.

Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Kilimo, Mohamed Chikawe Chikawe, alitoa wito huo jana jijini hapa, wakati akizindua uanzishwaji wa kituo cha mafunzo ya kilimo na biashara kilichofadhiliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya We- Effect, Oung World Feeders na Tanzania Youth Coalition.

Chikawe, alisema kilimo ni miongoni mwa sekta ambazo zina fursa nyingi za kuwasaidia vijana kujiajiri na kuajiriwa, badala ya kukaa kusubiri ajira serikalini.

"Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na vijana wanaojishughulisha katika sekta ya kilimo, kwa kuwa ni sehemu inayowapa ajira, niwaase wachangamkie fursa za taasisi na mashirika haya yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na sekta ya kilimo, ili kujiimarisha kwenye uchumi badala ya kusubiri ajira," alisema.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na vijana ambao wanajikita katika sekta hiyo, kwa kuwapatia mafunzo na vifaa, kwa ajili ya kuwawezesha kujiinua kichumi zaidi.

"Taasisi kama hizi zimekuwa zikitoa mafunzo kwa vijana kuhusu kilimo, ndiyo maana serikali imekuwa ikishirikiana, kwa kuwa imekuwa msaada katika kuisaidia serikali kuajiri," alisema Chikawe.

Mkurugenzi wa Tanzania Youth Coalition, Lenin Kazoba, alisema mashirika hayo yamekuwa yakifanya kazi kwa malengo kuwasaidia vijana ushauri juu ya kukuza kipato na kuwaunganisha na masoko.

"Mradi huu unalenga kuwafikia vijana zaidi ya 11,606 wakiwamo wanawake 6,606 na wanaume 5,000 ambao kwa kuanzisha kituo hiki vijana watapewa mafunzo ya nadharia za kilimo biashara na uongozaji wa thamani," alisema.

Kazoba, alisema kuwa We- Effect itawanufaisha vijana kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za kilimo endelevu, usimamizi wa biashara utunzaji wa mazao, baada ya mavuno, upatikanaji wa fedha matuminzi ya teknojia na uhifadhi wa mazingira ya kilimo yanayozingatia mabadiliko ya tabia nchi.

# Kilimo kidijitali kunufaisha wanawake, vijana 500,000

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAWAKE na vijana 500,000 wanatarajia kunufaika na kilimo, kwa ajili ya kuboresha maisha yao na kuondokana na umaskini.

Ni baada ya kunzinduliwa kwa mpango wa pamoja wa takwimu kwa mageuzi ya kilimo kidigitali nchini. Akizindua mpango huo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema utagharimu dola za Marekani milioni tatu na unalenga kutumia teknolojia kuleta mageuzi ya kilimo nchini.

Mweli, alisema programu hiyo inalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na ustahimilivu kwa jamii za vijijini hususani vijana na wanawake.

Alisema pia imelenga kuwasaidia kupata taarifa sahihi za upatikanaji wa masoko na kuimarisha mifumo ya kilimo wanachofanya.

Alisema mpango huo utatekelezwa kwenye mikoa ya Dodoma, Manyara, Kigoma na Ruvuma.

"Mpango huo unalenga zaidi wanawake na vijana, tunawashukuru wadau wa maendeleo, kwa kushirikiana na serikali kuinua sekta ya kilimo nchini," alisema Mweli.

**Mkuu wa Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Shabnam Mallick, alisema mpango huo unaungwa mkono na Umoja wa Ulaya (EU), kupitia Mfuko wa Pamoja ...**

Alisema hiyo ni hatua muhimu kuelekea kutimiza maono ya serikali ya kuendesha kilimo cha dijitali ambacho kitawawezesha wakulima wadogo kuimarisha mifumo ya chakula, ili kufikia Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Katibu Mkuu huyo, alisema sekta ya kilimo inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo uzalishaji mdogo, upatikanaji masoko, athari za mabadiliko ya hali ya hewa, hivyo programu hiyo, itawasaidia wakulima kupata taarifa hizo kwa wakati, ili kuchukua tahadhari pale inapobainika.

Mkuu wa Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Shabnam Mallick, alisema mpango huo unaungwa mkono na Umoja wa Ulaya (EU), kupitia Mfuko wa Pamoja wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Mallick, alisema programu hiyo itatekeleza matumizi ya majukwaa ya kidijitali kwa kutoa takwimu za kilimo kwa wakati, kusaidia wakulima wadogo kupata taarifa, kuboresha upatikanaji wa masoko na kuimarisha mifumo ya ufanyaji uamuzi.

"Mpango huu wa pamoja chini ya Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, utaanza kutekelezwa kwa kutoa takwimu za kilimo katika majukwaa ya kidijitali," alisema Mallick.

Aliahidi kuendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kutatua changamoto za kilimo kwa njia za ufumbuzi wa kibunifu, ili kuhakikisha sekta ya kilimo inakua kwa kasi kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.




Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Kilimo Mohamed Chikawe akizungumza na vijana wanaojishughulisha na sekta ya kilimo (hawapo pichani) baada ya kukizindua kituo cha mafunzo ya kilimo na biashara kilichofadhiliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya We- Effect,Oung World Feeders na Tanzania Youth Coalition katika hafla iliyofanyika Miyuji Dodoma jana.(kutoka kulia) Ray Mark Mkurugenzi Mtendaji wa Young World Feeders Foundation na Mkurugenzi wa taasisi ya Tanzania Youth Coalition Lenin Kazoba na (kushoto) Vumilia Zikankuba Mratibu wa BBT Wizara ya Kilimo. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Serikali kuimarisha uwekezaji nishati

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wafanyabiashara wa mafuta nchini kuwa, itaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji na miundombinu ya sekta ya nishati, ili kuwapa unafuu wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio katika hafla ya utoaji tuzo kwa mawakala na wadau wa uzalishaji mafuta wa Kampuni ya Puma Enegy Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, Dk. Mataragio aliipongeza kampuni hiyo, kwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kuhamasisha wananchi wanatumia nishati safi ya kupikia.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa Balozi na kinara katika kuhamasisha Watanzania watumie nishati safi ya kupikia nchini na duniani, ili kuhakikisha watu wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo yana madhara kwa afya na uharibifu wa mazingira," alisema Mataragio. Kuhusu tuzo hizo, Mataragia aliagiza ziwe chachu ya kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ufanisi kulingana na vigezo na masharti ya kampuni kwa maslahi ya Watanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Enegy Tanzania, Fatma Abdallah, alisema lengo ni kuimarisha uhusiano na kubadilishana mawazo kati ya menejimenti na mawakala.

Fatma, alisema wamezalisha ajira zaidi ya 1,000 na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Alisema sekta ya nishati ni chachu katika kuchochea maendeleo ya ukuaji uchumi na kwamba Rais Samia amekuwa kinara kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.



# Malori yafungwe vidhibiti mwendo - wadau

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeshauriwa kuyafungia vidhibiti mwendo malori, ili kupunguza ajali, vifo vya watu na uharibifu wa mali nchini.

Wadau walitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati wa mdahalo wa kujadili namna ya kupunguza ajali uliotishwa na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), kwa kushirikiana na Kamati ya Usalama Barabarani ya Mkoa.

Wadau hao wa usalama barabarani, walisema madereva wanaendesha malori hayo kwa mwendo kasi na kusababisha baadhi yao kushindwa kuyamudu na kusababisha ajali, ambazo zinagharimu maisha ya watu kwa kuwaua, kuwaacha na ulemavu na kuharibu mali.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, alisema malori yanakimbia kuliko mabasi, kutokana na kutokuwa na vidhibiti mwendo.

Mwalunenge, alisema wakati serikali inaanzisha utaratibu wa kufunga vidhibiti mwendo kwenye mabasi, iliaminika mwendokasi ndicho chanzo cha ajali hali ambayo sasa imehamia kwenye malori.

"Mimi mwenyewe nina malori ambayo yana uwezo wa kukimbia 'speed' (mwendokasi) wa kilomita 140 kwa saa, sasa ni vema tukaanza kufikiria kuyafungia vifaa hivi, ili kupunguza ajali," alisema.

Francis Almas, mmoja wa madereva walioshiriki mdahalo huo, alisema malori yamekuwa yakiendeshwa kwa mwendo kasi bila kujali eneo husika.

Alisema katikati ya Jiji la Mbeya kuna msongamano wa vyombo vya usafiri, zikiwamo bajaji na kuwa chanzo cha ajali, kutokana na baadhi ya madereva kukosa weledi.

**"Kati ya majeruhi hao, 650 walikuwa wameumia vibaya na walikuwa wanatakiwa upasuaji wa haraka, lakini takwimu hizi zilitushtua sana tukaona ni vema tushirikiane na wadau kujadili namna ya kupun-**

Alisema dereva wa lori anaweza akawa anaendesha kwa mwendo kasi na akawa salama, kwa sababu ana weledi, lakini tatizo likawa linaanzia kwa wa bajaji.

"Tunaomba sana hawa madereva wa bajaji wasiokuwa na weledi wadhibitiwe, wengine ni watoto na hawana hata leseni ila wanaendesha vyombo vya moto, hili ni tatizo ambalo limekuwa likisababisha ajali hapa kwetu," alisema Almas.

Mratibu wa Mdahalo huo kutoka hospitali hiyo, Emmanuel Makulila, alisema wameamua kuitisha mjadala huo, baada ya kupokea idadi kubwa ya majeruhi wa ajali za barabarani. Alisema katika kipindi cha miezi sita pekee hospitali hiyo ilipokea zaidi ya majeruhi 1,200 kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

"Kati ya majeruhi hao, 650 walikuwa wameumia vibaya na walikuwa wanatakiwa upasuaji wa haraka, lakini takwimu hizi zilitushtua sana tukaona ni vema tushirikiane na wadau kujadili namna ya kupunguza tatizo," alisema Makulila.

Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Anthony Mkwawa, alisema jeshi hilo limeyatambua maeneo yote ambayo ajali zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kuchukua hatua za kupunguza ajali hizo.

Alisema kwa sasa maeneo yote ya miteremko mikali malori na magari ya abiria yanapita kwa awamu, ili kupunguza madhara endapo ajali itatokea.

Akifungua mdahalo huo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wadau hao, kila mmoja kutimiza wajibu wake, ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Alilitaka jeshi hilo kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria madereva wazembe, ili kudhibiti ajali barabarani.



Baadhi ya wanawake wa Mkoa wa Mbeya, wakiwamo walimu wa Shule ya Msingi Mkapa ya jijini hapa, wakiwa wamembeba mmoja wa wanafunzi wa kike walioshinda tuzo kwenye mashindano ya kuandika insha, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha, ambayo kitaifa yalihitimishwa jijini humo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

## 'Wananchi waelimishwe kukuza uchumi'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI za fedha nchini zimetakiwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ya matumizi ya njia rasmi za fedha ili kukuza uchumia wao ifikapo mwakani.

Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja alitoa rai hiyo juzi jijini Mbeya wakati akifunga Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha kitaifa mkoani hapa.

Mwamwaja, alisema wananchi wengi hawatumii huduma rasmi za fedha kutokana na kukosa elimu sahihi, hivyo wadau wanatakiwa kuhakikisha wanaendelea kutoa elimu hiyo.

Alisema maeneo ya vijijini ni asilimia nane ya wananchi wanaotumia huduma rasmi za fedha.

"Wananchi wanachotaka ni elimu tu, wengine wanatamani kutumia hizi huduma lakini ndio hivyo hazipatikani katika maeneo yao, ni wajibu wenu kuhakikisha elimu hiyo inawafikia," alisema Dk. Mwamwaja.

Aliwataka wananchi walioshiriki maadhimisho hayo kuhakikisha wanatumia elimu waliyoipata kubadilika kwa kuanza kutumia huduma rasmi walizoelekezwa na wadau.

Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Janet Hiza, alisema katika maadhimisho hayo kulikuwa na mabanda ya zaidi ya taasisi 80 ambazo zilikuwa zinatoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya huduma rasmi za fedha.

Janet, alisema katika maadhimisho hayo, walipokea malalamiko na maoni kutoka kwa wananchi kwa ajili ya kuboresha huduma hiyo.

Lengo la serikali ni kuhakikisha asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia mifumo rasmi mwaka ifikapo mwaka 2025

# Wanawake walilia kituo cha afya Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE wa Kijiji cha Ukalawa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wameomba serikali kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya, ili kuwaondolea adha ya wajawazito kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda kujifungua.

Ombi hilo walilitoa mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya cha kijiji hicho, unaotekelezwa na Mfuko wa Mendeleo ya Jamii (TASAF) kwa zaidi ya shilingi milioni 157.

Wanawake hao, walisema huduma za afya zinapatikana katika Kata ya Lupembe, ambako ni mbali na kusababisha baadhi ya kushindwa kubeba ujauzito kwa kukosa mahali pa kujifungulia.

Mmoja wa wanawake hao, Vera Bebeta, aliomba huduma kuanza kutolewa kwa wakati.

Kalista Mhiche, alisema lengo kubwa la kuanzisha ujenzi wa kituo cha afya, ilikuwa kukabiliana na tatizo la wajazito kwenda kujifungua mbali na kusababisha vifo kwa baadhi yao na watoto kwa kukosa huduma mapema.

"Kituo hiki kikikamilika wakinamama tutajifungua kwa urahisi na kwa matumaini mkubwa hata vifo havitatokea tena," alisema Mhiche.

Diwani wa Ukalawa, Javan Ngumbuke, alisema tangu mwaka 2021 walianza ujenzi wa jengo la nje (OPD), ili kuwaondolea wananchi adha ya kutembea kilometa 30 kufuata huduma za afya na wajawazito kujifungulia njiani na wengine kupoteza maisha.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Njombe, Kelvin Kapungu, alisema wamepokea Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya kutekeleza za miradi ya mfuko huo.

Kwa upande wake, Mtaka aliumagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Dk. Frank Mganga, kuhakikisha huduma za afya zinazinduliwa Desemba 14, mwaka huu.

Mratibu wa TASAF wa Mkoa huo, Musa Seleman, alisema mwaka 2023 kulianzishwa mradi wa kilimo cha parachichi kwa wanufaika, ili kuwajengea uwezo kwa kujitegemea na kuondokana na umasikini.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Valentino Hongoli, alisema kituo hicho kikikamilika kitakuwa msaada kwa wananchi.





# ZLS yapewa rungu la watakaovunja katiba, sheria

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Wanasheria Zanzibar (ZLS) kimetakiwa kuzichukulia hatua mamlaka la taasisi za serikali zinazovunja katiba na kukiuka sheria za nchi.

Wito huo umetolewa na Makamu wa kwanza wa Rais Othman Masoud Othman wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka chama hicho uliofanyika visiwani Zanzibar.

Othman, alisema wananchi wanapokosa haki zao chama hicho kinapaswa kiwe kimbilio lao ili kuhakikisha zinalindwa kwa mujibu wa katiba na sheria.

"Chama cha wanasheria pale katiba ya nchi inapovunjwa na mtu au mamlaka yoyote kinastahiki kiwe mstari wa mbele kupaza sauti na kuchukua hatua stahiki," alisema Othman.

Alisema chama hicho kina wajibu wa kulinda haki za kiraia, ikiwemo kusimamia mashauri yenye maslahi ya umma ili kufikia misingi ya utawala bora.

"Ni kinyume na ni fedheha kubwa pale haki za kiraia zinapokuwa hatarini ama kwa sababu ya wenye mamlaka au maslahi ya kibiashara, sio vyema kwa chama cha wanasheria kuwa kimya na kutotimiza wajibu wa kupaza sauti tukifika hapo raia hawatakuwa na mlinzi madhubuti dhidi ya matumizi mabaya ya madaraka, kukosa uwajibikaji, ufisadi na dhulma za kimfumo au kiutendaji," alisema.

Aliwataka wanasheria kutenga muda maalum kwa ajili ya kutoa elimu ya uraia na msaada wa kisheria wananchi wanapokuwa na matatizo na kukoseshwa haki zao.

Akizungumzia uchaguzi mkuu wa 2025, Othman, alisema sio wa chama na wala si suala la kuamua masuala ya kisiasa bali ni mahakama ya wananchi kupata fursa kuamua hatma ya nchi yao.

Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, aliwataka wanasheria kufuata maadili ya kazi zao kwa kutenda haki na kujenga imani na serikali, kuikosoa na kuishauri.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha serikali ya umoja wa kitaifa na kuwataka wanasheria kuunga mkono juhudi hizo kwa manufaa ya wananchi.

Aliyekuwa Rais wa Chama cha Wanasheria, Masoud Rukazibwa, alisema wanakabiliwa na vikwazo vingi ikiwemo kukosa fursa ya kupewa kazi na serikali za kusimamia mikataba katika miradi ya maendeleo.

Alisema wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa rasilimalimaeneo ya vijijini.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto), akimkabidhi tuzo wakili wa Mahakama Kuu, Hassan Kijogoo, wakati wa mkutanomkuu wa mwaka wa Chama cha Wanasheria Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi kuendelea kuibadili Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameahidi kuendelea kuibadili Zanzibar kuwa kituo bora cha biashara cha kimataifa kwa kutoa fursa kwa wafanyabiashara mataifa mbalimbali dunidni kuuza na kununua bidhaa visiwani humo.

Dk. Mwinyi alifafanua kuwa ahadi yake hiyo inafuatia kuwekwa miundombinu imara ya masoko ya kisasa kutoa huduma za biashara kwa saa 24, kuboresha barabara kubwa na upanuzi wa viwanja vya ndege vyenye hadhi ya kimataifa Unguja na Pemba.

Dk. Mwinyi alitoa ahadi hiyo wakati akifungua soko jipya la ghorofa mbili Mwanakwerekwe lililopo Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwa ni mwendelezo wa mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) anayoiongoza.

Mwingine aliahidi kuunganisha huduma rahisi ya usafiri wa umma kwa kuagiza mamlaka zinazosimamia masoko kujenga vituo vikubwa vya mabasi kuruhusu muingiliano wa moja kwa moja baina ya masoko hayo ya Kwereke, Jumbi na Chuini ili kutoa fursa kwa wananchi na wafanyabiashaa kunufaika.

Akizungumzia mwenekano mpya wa haiba ya Zanzibar, Dk. Mwinyi ameahidi kuendelea kufanya mageuzi makubwa ya kubadili mandhari ya miji yote ndani ya mwaka mmoja ujao kwa kujenga madaraja mawili makubwa kwa mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja.

Alisema lengo ni kuruhusu mwingiliano rahisi wa mikoa hiyo kibiashara na utalii kwa kujenga barabara za juu kutoka Uzi Ng'ambwa Kaskazini Unguja hadi Charawe - Chwaka Mkoa wa Kusini Unguja ili kurahisiaha sekta ya usafiri na usafirishaji.

Alisema wakati umefika kwa Zanzibar kuwa na mageuzi makubwa hasa kwa viwanja vya ndege vya Abeid Amani Karume na Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kufanya matengenezo makubwa jengo la pili la abiria kuwa na hadhi ya kimataifa. Akizungumzia bandari jumuishi ya Maghapwani inayotarajiwa kuwa kichochezi kikubwa na kukuza biashara nchini, Dk. Mwinyi alisema ujenzi wake uko mbioni kuanza.

**Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali kuwaletea maendeleo.**

Wakati huo huo; Rais Mwinyi ameziagiza mamlaka zinazosoimamia Soko la Mwanakwerekwe kutowatoza ushuru mkubwa wafanyabiashara.

Alisema fedha zilizotumika kujenga soko hilo si mkopo bali kodi za wananchi, hivyo Serikali haitegemei chochote kutoka kwao na wafanyabishara wa soko hilo.

Alisema fedha watakazotozwa wafanyabiashara hao zitatumika kuendesha soko hilo na kulitunza.

Vilevile, aliwaagiza wanaosimamia soko hilo la Kwereke kufuata utaratibu kwa kuwazuia wafanyabiashara kufanya biashara kwenye hifadhi ya barabara na maeneo yasiyo rasmi.

Hata hivyo, Dk. Mwinyi alisema serikali yake itaendelea kuwaongezea mitaji ya biashara wafanyabiashara endapo watakuwa na utaratibu mzuri wa kujiunga kwenye vikundi.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali kuwaletea maendeleo.

Hata hivyo, Abdullah, alisema kufunguliwa soko hilo kutatoa zaidi ya ajira 100,000 na kuwanufaisha watu wengi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muhamed Mchengerwa, akizungumza kwenye ufunguzi wa soko hilo, alisifia michango ya viongozi wakuu wa nchi Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Mwinyi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo kama ilivyokuwa kwa waasisi wa taifa, Abeid Amani Karume na Baba wa Taifa, Julius Kambarage Nyerere.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kuwekeza katika mradi mkubwa wa soko hilo la Mwanakwerekwe na.

Ujenzi wa soko hilo lenye uwezo wa kuwahudumia wafanyabiashara zaidi ya 5,000 kwa wakati mmoja, umegharimu shilingi bilioni 35.8.

# Madaktari waonywa kudharau wagonjwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Wizara ya Afya, Hassan Khamis Hafedh ameonya kuwa Serikali ya Zanzibar itawachukulia hatua kali madaktari na watendaji wa vituo vya afya wanaodharau na kutoa lugha za kejeli kwa wagonjwa.

Hafedh alitoa onyo hilo wakati akifungua mkutano wa kikao kazi cha kuongeza ufanisi wa uwajibikaji kwa madaktari na wasimamizi hao visiwani hapa.

Alisema hatua hiyo imekuja kutokana na wananchi kuwalalamikia madaktari juu ya utendaji wao wa kazi wakati wanakwenda kupata huduma za afya kwenye vituo hivyo na hospitalini.

Alisema baadhi ya madaktari wanapokuwa katika hospitali za serikali na kituo cha afya hawawajibiki ipasavyo, katika hospitali binafsi wakuwa karibu na wagonjwa kwa vile wanalipwa fedha nyingi.

"Tunafahamu kuwa baadhi yenu mkiwa katika hospitali binafsi mnakuwa na heshima kwa wateja wenu ila kwa serikali mnadharau haipendezi, " alisema Hafedh.

Alisema serikali ikitumia fedha nyingi kwa ujenzi wa hospitali na vituo vya afya, hivyo ni wajibu kwa watendaji hao kufanya kazi kwa kufuata madili na misingi.

Alisema Zanzibar ni nchi ya kitalii imekuwa na wageni wengi mchanganyiko, suala la afya ni muhimu, hivyo kuna kila sababu ya watendaji wa sekta hiyo kujipanga kuhimiza usafi.

"Kisiwa hiki ni cha utalii watu mbalimbali wanakuja kutembelea hapa hivyo watalamu wa afya wanatakiwa kufanya kazi zao kwa kuelimisha usafi na huduma bora wanazotoa," alisema Hafidh.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Mngereza Mzee Miraji, alisema kikao hicho kina lengo la kukumbushana juu ya utendaji kazi kwa madaktari na wasimamizi wa vituo vya afya vya Unguja.

Miraji, alisema kuna malalamiko kutoka kwa wananchi ya utovu wa nidhamu kwa baadhi ya madaktari na watendaji, hivyo wizara imejipanga kuwachukulia hatua kali.

"Kila mtu anafahamu kuwa kuna malalamiko mengi kwa baadhi ya watendaji wa afya kuwadharau na kuwatolea maneno ya kejeli wagonjwa, jambo hili halikubaliki," alisisitiza.

Wajumbe wa kikao hicho, walisema kikao hicho kinaenda kuamsha ari ya utendaji kwa madaktari wa Zanzibar kutokana na umuhimu wao mkubwa kwa jamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**GEORGE.L.MPILI**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji TVS KING yenye namba za Usajili

**MC 472 BSM**

Atakaeiona atoe taarifa Kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi

**PHQ/DAR/KING/224018/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LUSAJO JUMA MWAKISAMBWE** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne, chenye index namba **S.1201/0242** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LUFILYO SECONDARY SCHOOL.** Mwaka 2023. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN//229423/2024**

**FOMU MADAI - 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**
**Shauri la Talaka No. 73/2024**
**Jina la Mwombaji: GERSHOM MWIDOWE**
**Jina la Mjibu maombi: JENIFER HANJE**

**KUITWA SHAURINI MJIBU MAOMBI**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: JENIFER HANJE**
**GEITA**

Kwa kuwa Mwombaji ameleta maombi yake kwamba Talaka, mgawanyo wa mali na matunzo ya mtoto.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 11 Mwezi 11 Mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 10 Mwaka 2024.

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE

## KUBADILISHA JINA

Katika Pasipoti yangu **N.V9541702**, jina la Mama yangu lilinakiliwa kimakosa kama **MEHJABI** ilhali jina sahihi ni **MAHAJABI.** Katika siku zijazo, mama yangu atajulikana kwa jina hili. Seyyad Raja Ali S/o Shah-anawaz Hussain R/o H.no .325 Budina Khurd P/S Titawi Tehsil & Distt Muzaffarnagar (UP).

## KUPOTEA KWA CHETI



**AFUA KASSIM MOHAMMED** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha sita chenye index namba S0738-0501 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RIDHWAA SEMINARY mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/228628/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF SHINYANGA**
**AT SHINYANGA**
**MISC/CRIMINAL/CIVIL/APPLICATION/PROBATE/MATRIMONIAL/EXECUTION/APPEAL NO.20501 OF 2024**
**ELIZABETH PETER..........APPLICANT**
**VS**
**DANIEL PETER...............RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

**To:...DANIEL PETER**

Take notice that the above Misc Applicatin is set for hearing at Shinyanga Distric Court.

You have attend before this Court on 14/11/2024 at 08:00 am to have it proceeded.

If you don't attend without cause and proper notification the case will be preceded in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court on 23 day of October 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
P.O.Box 29 - SHINYANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZINIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai /Ndoa Na. 419/2024**
**JINA LA MDAI............KENNETH EDWARD MLUGU**
**JINA LA MDAIWA............NOEL ANOLD LEMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA; NOEL ANOLD LEMA**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TSH. 25,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 31/10/2024 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 10 Mwaka 2024.

.................................................
**HAKIMU**

## KUFUNGA KAMPUNI

MKURUGENZI MTENDAJI **HASSAN ABDULLAHI JAMA** ANATANGAZA KUFUNGA KAMPUNI YA FIBO NIGHT-CLUB LIMITED. ILIYOPO JIRANI NA KITUO CHA POLISI NGARENARO ARUSHA CBD. YENYE TIN NO : **163-696-142.** ILISAJILIWA NA BRELA TAREHE 11 OCTOBER 2024 KWA NAMBA **163696142.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMEMTS ACT , CAP 117(R.E.2019)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**
**BY**
**ANNA KALEBI MBISE**

By this deed, **I ANNA KALEBI MBISE** of 0754-374982-Arusha Do hereby wholly and absolutely renounce, relinquish and abandon the use of my former name of ANNA DOMINIC MSANGI and in lieu thereof adopt as from the date of poll the name of ANNA KALEBI MBISE.

The reason for this change of name is I want to abandon my Husband's name ANNA DOMINIC MSANGI and use my biological Father's name ANNA KALEBI MBISE.

AND in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all public and private dealings and upon all occasions whatsoever use and subscribe the name of ANA KALEBI MBISE.

I hereby require and authorize all persons designate and describe me by the name of ANNA KALEBI MBISE.

In witness hereof I ANNA KALEBI MBISE have set my hand at Arusha this 19th day of February ,2024.

Sworn and Delivered at Arusha by the said
ANNA KALEBI MBISE who is known
To me personally/identified to me by......Deponent the later being known to me personally in my presence this 19th day of February,2024.



## KUPOTEA KWA CHETI



**JENIFA L JULIUS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye Index No. S2295-0504 .Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa MAIRIVA SECONDARY SCHOOL mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye . Polisi taarifa: **PHQ/ARU/B/40505/2024.**

## NOTISI YA TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ULIPAJI WA DENI PAMOJA NA MNADA WA HADHARA

Rejea tangazo la tarehe **21.10.2024** katika gazeti la Nipashe kuhusu mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa.

**SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd** Kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LTD** tunatangazia umma kuwa kuna marekebisho ya tangazo tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza na kuwa mdaiwa ndugu Samwel Ezekiel Masunga wa Dar es Salaam anatakiwa kulipa deni lake la mkopo analodaiwa ndani ya siku kumi na nne (siku 14) tangu siku ya tangazo kutoka gazetini. Vinginevyo **SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd** tutaendelea na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mkopo kama ratiba inavyoonyesha kwenye jedwali hapo chini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| SAMWEL EZEKIEL MASUNGA | Gari T.977 EEN TOYOTA HIACE - SEPCO Yard (Tabata) | 15/11/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |

**Masharti Mengine:**

Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: SEPCO: 0715683777**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: +255 - 0677 020701***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# BRICS waja na mfumo mpya malipo ya kifedha mpakani

**MOSCOW, RUSSIA**

UMOJA wa mataifa yanayochipukia kiuchumi (BRICS), umeanzisha mfumo mpya wa malipo katika mipaka ya nchi wanachama wake uitwao ‚BRICS Pay'

BRICS inaundwa na nchi za Brazil, Russia, India, China, Afrika Kusini, Iran, Misri, Ethiopia, Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E).

Kadi za malipo zitakazotumika katika mfumo huo, zilitolewa kwa washiriki wa kongamano lililofanyika kuanzia Oktoba 22 hadi 24, mwaka huu, nchini Russia.

Kadi hizo zilikuwa na thamani ya ruble 500 (Dola za Marekani 5.20) zilitumika katika majaribio kwa kununua viburudisho kama vile kahawa pamoja na zawadi ndogo kwenye mkutano huo.

Lengo kuanzishwa kwa mfumo huo wa malipo kupitia kadi ni kukabiliana na wasambazaji wa fedha kutoka Marekani pamoja na vikwazo dhidi ya kiwango cha juu cha deni la taifa la Marekani.

Pia ililenga kuzihimiza nchi wanachama wa BRICS, kuimarisha matumizi ya sarafu zao katika biashara za kimataifa.

Faida nyingine ya mfumo huo, ni kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi baina ya nchi wanachama na kuachana na matumizi ya dola pamoja na kuunda kanda ya biashara yenye ushirikiano zaidi.

Hatua hiyo pia inaonesha dhamira ya kundo hilo ya kupunguza utegemezi kwa Dola ya Marekani katika biashara ya kimatifa mwelekeo muhimu katika katika sekta ya fedha za kimataifa.

Wachambuzi wa masuala ya kimataifa wanasema mfumo huo wa malipo utaleta athari kubwa katika Dola na kuidhoofisha.

Wachambuzi hao wanapendekeza kwamba mfumo huo mpya utaleta mabadiliko makubwa katika miamala ya mipaka, kutumia teknolojia ya ‚block chain' na sarafu za kidijitali

Lakini mshauri wa usalama wa Marekani, Jake Sullivan anasema Marekani haiangalii BRICS kama mpinzani wa kiuchumi.

Nchi za BRICS zinaendeza kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kupitia miradi mbalimbali katika mkutano huo, walijadili pia uwezekano wa kuanzisha sarafu mpya ya akiba, jambo linaloashiria dhamira ya kubadilisha mfumo wa kifedha wa kimataifa

***AFP***



Marais Xi Jinping wa China, Vladimir Putin wa Russia na Waziri Mkuu wa India, Narendra Mudi wakitembea pamoja baada ya kumaliza mkutano wa BRICS uliofanyika katika mji wa Kazan, Russia wiki iliyopita. **PICHA: REUTERS**

# Idadi ya vifo vyaongezeka baada Israel kufanya mashambulizi Iran

**TEHRAN, Iran**

IDADI ya vifo kutokana na mashambulizi ya Israel ya kulipiza kisasi dhidi ya Iran, vimeongezena na kufikia wanajeshi wanne na wengine kadhaa wamejeruhiwa.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), lilisema lililenga viwanda vya makombora na maeneo mengine ya kijeshi karibu na jiji la Tehran na magharibi mwa nchi hiyo.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, ilisema kuwa mashambuzli hayo yaliyofanywa juzi na Israel nchi hiyo ina jukumu la kujilinda, lakini iilieleza kuwa Iran inatambua wajibu wake kwa amani na usalama wa ukanda huo.

Kulipiza kisasi kwa Israel kwa msururu wa makombora 200 ya balestiki yaliyorushwa kuelekea Israel, Oktoba Mosi, mwaka huu, yalikuwa yakitarajiwa kutokea wiki kadhaa.

Iran ilisema shambulio hilo lilikuwa la kulipiza kisasi mauaji ya kiongozi wa kisiasa wa Hamas, Ismail Haniyeh katika ardhi ya Iran, Julai.

Makombora mengi yalidunguliwa na Israel na washirika wake lakini idadi ndogo ilishambulia Israel ya kati na kusini.

Mamlaka ya Iran ilisema, maeneo katika mikoa ya Tehran, Khuzestan na Ilam yalishambuliwa.

Jeshi Iran lilieleza kuwa ilimefanikiwa kuzuia mashambulizi hayo, ingawa kulikuwa na uharibifu mdogo katika baadhi ya maeneo. Vyombo vya habari vya serikali ya Iran vilionesha kanda za video za msongamano wa magari kama kawaida katika miji kadhaa, huku shughuli za shule na michezo zikiripotiwa kufanywa kama ilivyopangwa.

Jeshi la Israel lilitangaza operesheni ya Jumamosi muda mfupi baada ya kuripotiwa milipuko nchini Iran.

Msemaji wa IDF, Daniel Hagari, alisema jeshi limeonyesha kujitayarisha kulinda taifa la Israel. Pia alionya ikiwa Iran itaanzisha duru mpya ya kuzidisha mashambulizi, basi Israel italazimika kujibu.

***BBC***

## Uingereza yabanwa fidia biashara ya utumwa

**APIA, Samoa**

NCHI 56 za Jumuiya ya Madola, zimekubaliana kwamba umefikia wakati wa mazungumzo juu ya biashara ya utumwa.

Tamko hilo limefikiwa wakati wa kilele cha mkutano wa jumuiya hiyo, ambao ulitawaliwa na wito wa Uingereza kutoa fidia kwa nchi zilizoathirika.

Viongozi wa nchi hizo, pamoja na wa Uingereza walifanya mazungumzo marefu na yenye utata kuhusu vipengele nyeti vinavyohusu historia yao.

Katika taarifa ya pamoja, viongozi wa Jumuiya ya Madola, walitilia maanani wito wa fidia uliosababishwa na watumwa waliopelekwa nje ya nchi zao.

Viongozi hao pia wamezungumzia juu ya athari za kudumu zilizotokana na wenyeji wa maeneo kadhaa, kuporwa umiliki wa raslimali zao na wakoloni.

Katika tamko hilo viongozi wa nchi za jumuiya ya madola walisema wakati umefika wa kufanya mazungumzo ya dhati kwa lengo la kujenga mustakabali wa pamoja katika msingi wa haki.

Mataifa ya Kiafrika, Caribbean na Pasifiki yanaitaka Uingereza na mataifa mengine yaliyokuwa na makoloni yalipe fidia, kwa kuendesha biashara ya utumwa na kwa ukoloni uliyosababisha matatizo mengine.

Nchi hizo zinataka mazungumzo yafanyike kuhusu fidia.

Nchi nyingi zimeendelea kuwa maskini zaidi kuliko nchi za wakoloni wao na bado zinaendelea kukabiliwa na athari zilizotokana na biashara ya utumwa.

Watu kati ya milioni 10 hadi milioni 15 kutoka bara la Afrika, walichukuliwa na kugeuzwa watumwa kwa muda wa karne nne.

Licha ya Uingereza kuonesha majuto kutokana na kadhia hiyo, mpaka sasa inapinga wazo la kulipa fidia ya fedha zinazoweza kuwa kiasi kikubwa.

Wakati wa mkutano huo, Uingereza ilijaribu kuepuka kutoa ahadi za wazi sambamba na kujaribu kuonesha nia ya kudumisha umoja huo.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Keir Starmer, alieleza kwamba mkutano wa huo haukuzungumzia kuhusu fidia.

Alisema msimamo wa nchi yake uko wazi juu ya suala hilo la fidia.

Viongozi wa nchi za jumuiya hiyo, walichelewa kutoa tamko la pamoja kutokana na majadiliano ya kutafuta mwafaka.

Waziri Mkuu wa Bahamas, Philip Davis; alisema wakati umefika wa kuwapo mdahalo wa dhati juu ya udhalimu uliofanyika.

***DW***

# MAKAMU WA RAIS KUSHIRIKI TIGO Z'BAR MARATHON 2024

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, anatarajiwa kushiriki mbio za Tigo Zanzibar Marathon 2024, zitakazofanyika mwezi ujao visiwani humo.

Aidha, amepongeza waandaaji wa mbio hizo ambazo amezitaja zinaunganisha watu.

"Binafsi napenda sana kushiriki katika mbio hizi, zinawaleta watu pamoja na kushiriki katika kujenga afya, nawapongeza sana waandaaji na wadhamini wa mbio hizi," alisema.

Alisema mbio hizo ziendelee kuwa endelevu na kuboreshwa zaidi kila mwaka ili ziwavutie watu wengi zaidi.

"Mungu akitupa uhai na uzima safari hii na mimi nitashiriki, nilikuwa sijawahi kushiriki kwa sababu mbalimbali, napata mwaliko, lakini kwa sababu zilizo nje ya uwezo wangu, sikupata nafasi, mwaka huu nitashiriki," alisema.

Akizungumzia mbio hizo, mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Tigo Zantel Kanda ya Zanzibar, Azizi Said Ali, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na tayari watu wameanza kujiandikisha kwenye vituo mbalimbali, Dar es Salaam na visiwani humo.

Alisema mwitikio umekuwa mkubwa na wanaamini idadi itaongezeka kwa watu kushiriki zaidi katika msimu huu wa tatu wa Tigo Zanzibar Marathon.

"Tunaendelea na maandalizi, na kwa kweli yanaenda vizuri sana, tunatarajia wanariadha na watu mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kuja kushiriki," alisema Ali.

Alisema kwa mwaka huu mbio hizo zitakuwa kuanzia kilometa tano, 10 na kilometa 21 (nusu marathon)

Mbio hizo zinazodhaminiwa na Kampuni ya Tigo, zinafanyika kwa msimu wa tatu mfululizo.

**POKEA MAUA YAKO...**



Balozi wa India nchini, Bishwadip Dey (wa tatu kushoto), akimkabidhi zawadi ya ua mwanamuziki wa kimataifa, Subhash Goyal, kutoka nchini India, baada ya kutoa burudani pamoja na kundi lake la Bollywood Rockers, kwenye Kituo cha Utamaduni cha Swami Vivakananda, Masaki jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Geita Gold mbabe wa Mtibwa Championship

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kucheza michezo mitano bila kupoteza, hatimaye Mtibwa Sugar, juzi ilipata mbabe wake kwenye Ligi ya Championship, ilipochapwa bao 1-0 dhidi Geita Gold, katika mchezo mkali na wa kusisimua uliopigwa, Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Mechi hiyo ilikumbushia enzi zao zilipokuwa Ligi Kuu Tanzania Bara, kwani zote ziliteremka msimu uliopita, hivyo kuwa ni mechi yenye upinzani mkali.

Bao pekee la ushindi la Geita Gold lilifungwa na straika wa zamani wa Stand United, Ndanda, Simba, KMC, Polisi Dodoma na Mtibwa Sugar yenyewe, Vitalisy Mayanga, dakika ya 38, ambaye alipiga mpira kwa kichwa cha kuchupa kutokana na mpira uliorushwa na beki wa zamani wa Yanga, Abdulaziz Makame.

Kipigo hicho si tu kwamba kinahitimisha Mtibwa Sugar kucheza michezo mitano bila kupoteza, lakini kimeishusha kutoka nafasi ya kwanza mpaka ya pili.

Ushindi huo unaipeleka Geita Gold kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ikifikisha pointi 14 kwa michezo sita iliyocheza, ikishinda minne na sare miwili, huku Mtibwa ikisalia na pointi 13 kwa michezo sita, ikishinda minne, sare moja na kupoteza mmoja.

Kwingineko, Maafande wa Polisi Tanzania waliendeleza ubabe wao baada ya kuichapa African Sports bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ushirika, Kilimanjaro ambao umeipeleka hadi nafasi ya saba ya msimamo ikifikisha pointi nane, ikiiacha African Sports hoi kwenye nafasi ya 15 na pointi yake moja kwa michezo sita iliyocheza.

Kwenye Uwanja wa Sokoine, wenyeji, Mbeya City walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mbuni, lililowekwa ndani ya wavu na Andrea Kihumbi dakika ya 39 ya mchezo.

Ushindi huo unaipandisha Mbeya City hadi nafasi ya tano, ikifikisha pointi 11, huku Mbuni ikisalia na pointi sita ikiwa nafasi ya 11 ya msimamo.

## Kocha wa Mlandege alia na mastraika

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mdaidizi wa timu ya Mlandege FC, Sabri China, ameendelea kudai kuwa suala la umakini kwa wachezaji wake ni 'mzimu' usiokwisha.

Sabri alisema bado wanasaka mwarobaini wa tatizo hilo ili kuhakikisha wachezaji wanafanya vizuri katika michezo migumu iliyo mbele yao.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Sabri alisema safu yake ya ushambuliaji inafanya vizuri mazoezini, lakini inashindwa kufanya vizuri katika mechi uwanjani.

Alisema bado wao kama benchi la ufundi wanatafakari namna gani wataweza kulitatu suala hilo hasa kwa nafasi ya ushambuliaji ambayo ndio inayompa maumivu.

"Bado nalia na umakini unatokana na wachezaji kushindwa kutulia kwa mujibu wa nafasi zao, wanacheza jazba sana kadri wanaposhindwa kutumia nafasi, hivyo bado tunakazi katika somo hili," alisema Sabri.

## Ngara watakiwa kuzingatia mazoezi

**Na Judith Julius, Ngara**

MKUU wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Julius, amewataka viongozi mbalimbali wilayani hapa kuhamasisha wananchi kushiriki mara kwa mara mbio za mwendo wa pole pole.

Julius alisema hayo aliposhiriki katika mbio hizo wilayani hapa Jumamosi iliyopita.

Mbio hizo zilitumika kuhamasisha wananchi kujiandikisha kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Aliwataka viongozi hao wa wilaya kuhakikisha kuwa mbio hizo haziishii kuhamasisha uandikishwaji, akisisitiza ushiriki katika mbio hizo unapaswa kuwa endelevu.

Afisa Utamaduni, Sanaa, na Michezo wa Wilaya ya Ngara, Saidi Salim, yeye aliwasihi washiriki wa mbio hizo waliojitokeza kwa wingi kuwa ushiriki huo katika mbio hizo uwe endelevu wilaya mzima.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BALOTELLI HUYOOO GENOA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Italia, Mario Balotelli mwenye umri wa miaka 34, anakaribia kujiunga na Genoa ya Serie A kama mchezaji huru. ***(Sky Italy)***

### CHILWELL KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inaweza kumnunua beki wa kushoto wa England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 27 kutoka Chelsea Januari. ***(Inside Track podcast, via Team talk)***

### MUSIALA KUONGEZA MKATABA

KUONGEZA mkataba wa kiungo mkabaji Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21, ambao unadumu hadi 2026, ni kipaumbele kwa Bayern Munich. ***(Bild)***

### DORTMUND HAINA MPANGO

KLABU ya Borussia Dortmund kwa sasa haina mpango wa kuchukua nafasi ya Nuri Şahin kama kocha licha ya klabu hiyo kuwa katika nafasi ya saba kwenye Bundesliga kutokana na kufungwa Jumamosi na Augsburg. ***(Sky Germany)***

### GUEHI BASI TENA PALACE

CRYSTAL Palace inasitasita kuanzisha tena mazungumzo na Newcastle United kuhusu mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### LUCCA ATAKIWA JUVE

JUVENTUS iko tayari kufanya mazungumzo mapya na Udinese kuhusu mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Italia, Lorenzo Lucca, 24. ***(Rudy Galetti)***

### RAPHINHA MKATABA MPYA

BARCELONA wanaamini kwamba mkataba mpya na winga wa Brazil, Raphinha utafanyika. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, utaendelea hadi 2027. ***(Diario Sport)***

### PEDRI MAMBO SAFI

MAJADILIANO kuhusu mkataba mpya kati ya kiungo wa kati wa Barca na Hispania, Pedri mwenye umri wa miaka 21, yanaendelea vema. ***(Fabrizio Romano)***

### COSTA ATAKIWA BARCA

BARCELONA wana nia ya kumsajili mlinda mlango wa Porto ya Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 25, ambaye pia anasakwa na Manchester City, lakini kitita cha kumsajili kilichoongezeka hadi euro milioni 45 kinafanya dili hilo kuwa gumu. ***(Sport)***

### SEMENYO AWINDWA EPL

FOWADI wa Ghana, Antoine Semenyo, alitia saini kuongeza mkataba wake msimu wa majira ya joto, lakini klabu kama Newcastle United na Tottenham Hotspur, zinazomuwinda huenda zikaona ofa ya Bournemouth kwa mchezaji huyo wa miaka 24 kama mpango mwingine wa kumbakisha katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# YAMAL AVUNJA REKODI YA MIAKA 77 CLASICO

## Ni wakati wakiitandika Real Madrid mabao 4-0 na yeye kuwa mchezaji ambaye ni...

**MADRID, Hispania**

MCHEZAJI wa maajabu wa Barcelona, Lamine Yamal, ameweka rekodi ya kuwa mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya El Clasico wakati timu yake ilipoichakaza Real Madrid kwa mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Bernabeu, Jumamosi usiku.

Barca walikuwa na wakati mgumu kipindi cha kwanza kabla ya kutoka nje ya mitego mwanzoni mwa kipindi cha pili na mabao mawili ya haraka ya Robert Lewandowski yakawaweka kwenye udhibiti kamili.

Vinara hao wa LaLiga walilinda bao lao vema na kuongeza bao katika dakika ya 77 wakati Yamal alipochombeza upande wa kulia na kuubetua mpira juu ya golikipa, Andriy Lunin na mpira kuja wavuni.

Hiyo ilimaanisha kwamba, Yamal alikua mfungaji mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kufunga katika historia ndefu kwenye mchezo wa Clasico akiwa na miaka 17 na siku 105, akiipiku rekodi ambayo iliwekwa miaka 77 iliyopita.

Alfonso Navarro ndiye aliyekuwa mfungaji mdogo zaidi, baada ya kuifungia Barca mabao mawili dhidi ya Madrid akiwa na umri wa miaka 17 na siku 365 mwaka 1947.

Baada ya bao hilo kikosi cha Carlo Ancelotti kikajikuta tena kwenye wakati mgumu, wakati Raphinha alipokimbia na mpira na kumpita kipa Andriy Lunin na kubadili matokeo kuwa 4-0 na kufanya usiku wa kusikitisha sana kwa mabingwa hao wa Hispania na Ulaya.

Yote yalikuwa tabasamu kwenye kambi ya Barca, baada ya Hansi Flick kutoka kusimamia ushindi wa 4-1 dhidi ya klabu yake ya zamani ya Bayern Munich Jumatano na alikuwa akijiandaa kwa mchezo wa pili mkubwa katika muda wa wiki moja na safari ya kuelekea mji mkuu wa taifa hilo.

Ushindi huo uliowapeleka pointi sita juu ya Madrid kileleni mwa jedwali baada ya mechi 11.

Barca walishinda taji la LaLiga mwaka 2020, ambalo lilikuwa chini ya Xavi Hernandez msimu wa 2022/23, lakini sasa wana jukwaa zuri la kujenga kwa kushinda Bernabeu kwa mara ya kwanza tangu 2022, wakati Pierre-Emerick Aubameyang, Ronald. Araujo na Ferran Torres walipofunga.

HABARI MICHEZO

# Alexander-Arnold: Naitaka Ballon d'Or

**LIVERPOOL, England**




MCHEZAJI wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold, amesema anataka kuwa beki wa pembeni wa kwanza kushinda Ballon d'Or na kukumbukwa kama "beki bora wa kulia kuwahi kutokea kwenye soka".

Hakuna beki wa pembeni aliyeshinda tuzo ya mchezaji bora wa dunia, ambayo ilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1956.

Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26, alisema atachagua kushinda Ballon d'Or badala ya Kombe la Dunia.

"Naamini ninaweza," alisema Alexander-Arnold akiiambia Sky Sports.

"Nataka kuwa beki wa pembeni wa kwanza kuwahi kufanya hivyo.

"Ni asubuhi tu baada ya kustaafu kwamba unaweza kutazama kwenye kioo na kusema, 'Nilipata kila kitu .

"Haijalishi umeshinda mataji mangapi, au una medali ngapi. Ni muhimu unatoa nini kwenye mchezo na ikiwa utafikia uwezo wako kamili."

Gwiji wa Real Madrid Roberto Carlos, ambaye alicheza nafasi ya beki wa kushoto, alikuwa wa pili katika tuzo ya Ballon d'Or ya 2002, ambayo ilitwaliwa na mchezaji mwenza wa Brazil Ronaldo baada ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka huo.

Mabeki wawili wa pembeni wameteuliwa kuwania tuzo ya Wanaume 2024 ni beki wa Real Madrid, Dani Carvaja na Alejandro Grimaldo wa Bayer Leverkusen.

Sherehe ya kutoa tuzo hiyo inafanyika leo, Jumatatu.

# Man Utd, Madrid na Man City wagombea nyota Argentina

**MANCHESTER, England**



MANCHESTER United wanapigiwa upatu kumnunua kinda wa River Plate, Franco Mastantuono katika dirisha la usajili la Januari, litakapofunguliwa.

Mastantuono alikuwa na umri wa miaka 16 pekee, alipokuwa mfungaji mabao mdogo zaidi kwa River Plate, Februari mwaka huu, na kuibuka haraka kama mchezaji anayevutiwa na baadhi ya klabu kubwa barani Ulaya.

Miamba hao wa Argentina haraka walichukua tahadhari, ili wasijiachie katika hatari ya kupunguzwa kwa bei ya uhamisho na wakamhakikishia Mastantuono mkataba wa miaka miwili hadi Desemba 2026 na kifungu cha kutolewa cha euro milioni 45.

Real Madrid, wamekuwa wakihusishwa sana na kiungo huyo mkabaji mwenye umri wa miaka 17, huku ripoti kutoka Hispania wakati wa majira ya kiangazi zikidai kuwa masharti kibinafsi tayari yamekubaliwa kutokana na mazungumzo yaliyoongozwa na skauti mkuu mashuhuri, Juni Calafat.

Lakini Manchester City pia inasemekana kuwa kwenye nia ya kutaka kupindua meza na kumsajili.

ESPN Argentina sasa pia imeiweka Man United katika mbio za kuwania saini ya nyota huyo.

Ikiwa United, au klabu yoyote itafanikiwa, Mastantuono atalazimika kubakia Argentina kwa angalau miezi michache zaidi.

Sheria za FIFA haziruhusu uhamisho wa kimataifa wa wachezaji walio na umri wa chini ya miaka 18, isipokuwa kama familia yao itahama kwa sababu zisizo za soka.



# ANCELOTTI AELEZA SABABU MADRID KULA MABAO 4-0

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti, amedai Real Madrid haikustahili kuchapwa vikali hivyo na Barcelona kwenye El Clasico Jumamosi usiku na kutoa ukumbusho wa mafanikio ya awali ya timu yake, licha ya kushindwa vibaya.

Barcelona walipata ushindi wao wa kwanza ugenini kwenye Uwanja wa Bernabeu tangu mwaka 2022, huku mabao mawili ya Robert Lewandowski yakikishangaza kikosi hicho kilichokuwa nyumbani.

Lamine Yamal na Raphinha waliongeza mabao mawili zaidi na kufanya safu ya mabao kuwa mbaya sana kwa Madrid, ambao sasa wako pointi sita nyuma ya wapinzani wao hao wakubwa katika mbio za ubingwa wa LaLiga.

Ina maana 'Los Blancos' wana kazi nyingi ya kufanya, ili kutetea ubingwa, lakini Ancelotti alikuwa mwepesi kuwatetea wachezaji wake na kuangazia njia yao ngumu ya kupata utukufu siku za nyuma.

Alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari, baada ya mechi: "Matokeo hayaakisi kile kilichotokea. Walistahili kushinda lakini ulikuwa mchezo wetu.

"Tunapaswa kujifunza kutokana na hili. Kujikosoa ni jambo la msingi. Lakini hatutupi kila kitu kwenye pipa - kipindi chetu cha kwanza kilikuwa kizuri.

"Mara ya mwisho tulipoteza 4-0 nyumbani kwa Barcelona, tulishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hatutaacha kupigana."

Madrid wameshindwa kusonga mbele licha ya kumuongeza Kylian Mbappe kwenye kikosi chao wakati wa majira ya joto na walihitaji ufufuo wa kipindi cha pili, ili kuifunga Borussia Dortmund katika Ligi ya Mabingwa katikati ya wiki.

Mbappe alitatizika katika mechi yake ya kwanza ya El Clasico, akipotea kwa kuotea mara nane, huku Vinicius Junior, akikosa nafasi nzuri katika kipindi cha kwanza.

HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS NA SENEGAL ZAJIWINDA KWA WAFCON

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kukutana na Senegal katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo, nchini Morocco.

Twiga Stars inacheza mechi ya pili ya kirafiki ya kimataifa, baada ya mchezo wake uliotangulia dhidi ya Morocco, kumalizika kwa kupokea kichapo cha mabao 4-1.

Bao pekee la Twiga Stars katika mechi hiyo ya juzi, lilifungwa na Enekia Lunyamila, ambaye anacheza soka la kulipwa katika Klabu ya Mazatlan iliyoko Mexico.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Hilda Masanche, alisema jana, ameyafanyia kazi makosa waliyofanya katika mechi ya kwanza, lakini pia ameimarisha katika maeneo ambayo walifanya vizuri.

Masanche alisema timu yake imepata kipimo kizuri kwa ajili ya kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), zitakazofanyika kuanzia Julai 6 hadi 26, mwakani.

Kocha huyo alisema wapinzani wao Morocco wana uzoefu, lakini amewapongeza wachezaji wake kwa kuonesha kiwango kizuri licha ya kukubali kufungwa.

"Kiufundi tulitumia mechi ya jana (juzi), kama darasa na namna tutakavyojiimarisha kuelekea michuano ya WAFCON, ni mechi nzuri kwetu kwa ajili ya kujifunza, tunaangalia tulipokosea, ili kuparekebisha lakini kulinda kile ambacho tulifanya vizuri," alisema Masanche.

Aliongeza mechi ya leo dhidi ya Senegal wanatarajia utakuwa mchezo wa kutumia nguvu na akili zaidi, kwa sababu ya aina ya uchezaji wa mpinzani wao.

Alisema pia bado wanaendelea kuwajenga wachezaji wao ambao kwa sasa kuna mchanganyiko wa nyota wapya na wale wazoefu katika kikosi hicho.

## HUPATI KITU HAPA...



Mshambuliaji wa Real Madrid, Kylian Mbappe, akijaribu kufunga bila mafanikio baada ya kipa wa Barcelona, Inaki Pena, kuwa makini kuucheza mpira kwenye mechi hiyo ya LaLiga iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu usiku wa kuamkia jana na Barca kushinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# KMC yafichua siri Prisons kupoteza mechi tatu kwao

**Na Adam Fungamwango**

MAAFANDE wa Prisons, juzi walipoteza mechi ya tatu mfululizo wakiwa nyumbani, Uwanja wa Sokoine Mbeya, huku Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moalin, akisema ukitaka kuizuia timu hiyo ni kuwatengeneza wachezaji wapambane nao kwa mipira mirefu ya juu.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoisha kwa KMC kupata ushindi wa mabao 2-1, ikiwa ugenini, alisema waliinyima nafasi Prisons kucheza mipira yao ya pasi ndefu za juu.

"Prisons ni timu nzuri hasa inapocheza nyumbani, wachezaji wangu wamecheza kwa maelekezo niliyowapa, nawapongeza, tuliinyima nafasi kucheza mpira wao wa pasi ndefu za juu, ukitaka kuimaliza timu hii dili na mipira hiyo, hilo nililiona kwenye michezo yao iliyopita na nikawapa kazi wachezaji wangu waifanye na wameifanya kikamilifu," alitamba kocha huyo.

Mabao yote ya KMC yalifungwa na straika Deruweshi Saliboko dakika ya 16 na 60, huku Oscar Mwajanga akiifungia Prisons bao la kufutia machozi.

Ushindi huo unawapeleka KMC hadi nafasi ya nane ya msimamo ikifikisha pointi 11, ikiwa imeshacheza michezo tisa, ikishinda mitatu, sare mbili na kupoteza minne.

Ofisa Habari wa Prisons, Bright Mbwilo, alionesha kushangazwa na timu yake kuruhusu mabao ya haraka kwenye michezo mitatu iliyocheza.

"Ni mechi ya tatu sasa tunafungwa mabao kwenye robo ya kipindi cha kwanza, tunarekebisha, lakini inajitokeza tena, najua ni mchezo wakati mwingine bahati haiwi kwetu," alisema afisa habari huyo.

Mara ya mwisho Prisons kushinda ilikuwa ni Oktoba Mosi, mwaka huu, ilipoichapa Fountain Gate mabao 3-2 kwenye uwanja huo, lakini baada ya hapo ilipokea vipigo vitatu mfululuzo, ambapo mbali na cha jana, ilifungwa 2-0 dhidi ya Azam FC, Oktoba 18, kabla ya kudunguliwa bao 1-0 dhidi ya Simba, Oktoba 22.

Kipigo hicho kinaifanya Prisons kusalia nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi saba kwa michezo tisa iliyocheza.

Imeshinda mchezo mmoja tu, ikitoka sare nne mpaka sasa, huku ikijiandaa kucheza dabi ya Mbeya, Novemba 3, mwaka huu, dhidi ya KenGold.

## Simba haitaki kupoa, yavuta kiungo Uturuki

INATOKA UK. 24

dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba mwaka huu hadi Januari, mwakani.

"Si kwamba Yanga ni bora kuliko sisi, bali wana uzoefu tu, tunapaswa kuimarisha kikosi chetu na tunafahamu dirisha dogo lipo jirani, hivyo tutapaswa kuboresha zaidi kikosi chetu kwa kuwa mbio za ubingwa bado zipo wazi," alisema.

Kabla hata dirisha dogo halijafunguliwa, tayari Simba imeshamaliza na winga, Elie Mpanzu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambaye amekuwa akifanya mazoezi na kikosi hicho siku zote kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikiri kuwa dirisha dogo kutakuwa na ongezeko la wachezaji wachache, lakini wenye tija na uwezo mkubwa, ila bado muda haujafika wa kulizungumzia hilo, badala yake akili zao kwa sasa zipo kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Gamondi naye alia uwanja, waamuzi

INATOKA UK. 24

fanya yalitufanya kuwe salama zaidi, tulitengeneza nafasi na kufunga bao lingine," alisema Gamondi.

Kocha mpya wa Coastal Union, Juma Mwambusi, ambaye alikuwa benchini kwa mara ya kwanza, aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana, akisema Yanga walinufaika na ubora wa mchezaji mmoja mmoja.

"Nashukuru wachezaji wangu wamepambana sana, tumepoteza nafasi mbili za wazi kipindi cha kwanza, hawakuwa makini, niliwaambia kuwa watulivu wanapofika langoni, lakini naona bado, hili ni lazima nilifanyie kazi.

"Yanga wametumia ule ubora wa mchezaji mmoja mmoja kuamua matokeo, vinginevyo hii mechi ingeisha kwa sare, tumekubali, nitakwenda kukaa na wachezaji, ili kukiboresha kikosi," alisema Mwambusi.

Kuhusu hali ya uwanja, alisema ulikuwa sawa na wala haoni tatizo na hivyo ndivyo viwanja vya Tanzania vilivyo.

"Uwanja uko sawa, hivi ndivyo viwanja vyetu na wao wameshinda kwenye uwanja huu huu, wangefungwa sijui wangesemaje," alisema kocha huyo.

Ushindi huo umewapeleka Yanga nafasi ya pili ikifikisha pointi 21, ikicheza michezo saba ikishinda yote, bila kuruhusu bao, huku Coastal, ikiwa nafasi ya 11, ikikusanya pointi nane kwa michezo tisa iliyocheza, ikishinda miwili, sare miwili na kupoteza mitano.

Michezo

Jumatatu Oktoba 28, 2024

Nipashe

## Ancelotti aeleza sababu Madrid kula mabao 4-0

UKURASA 22



CHA NNE HICHO...



Winga wa Barcelona, Raphael Dias Belloli maarufu Raphinha (kushoto), akiifungia timu yake bao la nne huku kipa wa Real Madrid, Andriy Lunin na beki wa timu hiyo wakiwa kuokoa bila mafanikio. Katika mechi hiyo ya LaLiga iliyopigwa Uwanja Santiago Bernabeu usiku wa kuamkia jana, Barca ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA HAITAKI KUPOA, YAVUTA KIUNGO UTURUKI

## Fadlu asema anataka wapya watatu dirisha dogo huku Mukwala sasa akihamishiwa...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu yao ikiendelea kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, viongozi wa Simba bado hawajaridhika, kwani wanatajwa kumfuata kiungo mshambuliaji Foday Trawally raia wa Gambia, anayekipiga Klabu ya Cetinkaya TSK ya Uturuki.

Habari zilizopatikana jana kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema mazungumzo baina ya pande mbili yameshaanza na Simba inataka kumpa mkataba wa miaka mitatu mchezaji huyo mwenye miaka 23, ambaye pia ameshazichezea klabu mbalimbali nchini Uturuki, ikiwamo Tuzlaspor FC.

Chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo kinasema kuwa Simba imeamua kuongeza kiungo mshambuliaji anayichezea klabu hiyo iliyopo Ligi Draaja la Pili nchini humo, ili kuwasaidia wachezaji wawili kwenye eneo hilo ambao ni Jean Charles Ahoua na Awesu Awesu.

„Ni usajili unaotokana na matakwa ya kocha, amesema anahitaji dirisha dogo waingie wachezaji watatu wa viwango vya juu vya kimataifa kwa ajili ya mechi kubwa.

“Mchezaji huyu ni kiungo mshambuliaji, ambaye kazi yake itakuwa ni kusimama nyuma ya washambuliaji, kutengeneza nafasi na kutoa pasi za mwisho.

„Skauti yetu imejiridhisha kuwa ni mchezaji bora na anayefaa kwa kazi hiyo, kocha anahitaji kiungo anayetengeneza nafasi rahisi zaidi kwa mastraika na huyu ndiye chagua,“ kilisema chanzo hicho.

Mbali na mchezaji huyo, habari zinasema Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, anahitaji pia beki wa kati ambaye ni mrefu na mwenye nguvu kwa ajili ya michezo migumu ya kimataifa kwani anadai mabeki wake tegemeo ni wafupi, hivyo anayekuja anaweza kumsaidia kwa kiasi kikubwa kutengeneza ukuta imara zaidi.

Chanzo kinasema kuwa Fadlu anahitaji pia viongozi kwenda sokoni kusaka straika mmoja ili kusaidiane na Leonel Ateba, huku akipendezwa zaidi uchezaji wa Steve Mukwala uhamie pembeni.

“Kocha anasema anataka Mukwala awe anacheza kama winga kwa sababu ni msumbufu, anakaba, ana mbio na uwezo wa kupiga krosi zenye usahihi na za hatari, kwa hiyo anataka kumhamisha ingawa kuna mechi bado atakuwa akimtukia kama straika wa kati,“ alisema mtoa taarifa.

Mara baada ya mchezo kati ya Simba na Yanga uliopigwa Oktoba 19, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Fadlu alifichua lengo lake la kutaka kukiimarisha kikosi chake kipindi cha dirisha

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi naye alia uwanja, waamuzi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameulalamikia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha, akisema hauko kwenye ubora, huku akisema viwanja vitatu tu vinavyobeba taswira ya soka la Tanzania ni ule wa Benjamin Mkapa, Azam Complex, ambavyo vyote vipo, Dar es Salaam na New Amaan Complex, Zanzibar.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake na Coastal Union, akiibuka na ushindi wa bao 1-0 lililowekwa wavuni na Jean Baleke, Gamondi amesema, baadhi ya viwanja ni vibovu kiasi kwamba vinasababisha timu zicheze mpira wa kubutuabutua kitu ambacho si picha nzuri kwa Ligi ya Tanzania.

„Pointi hizi tatu ni muhimu sana kwetu katika mwendelezo wa kupigania nafasi ya kutwaa ubingwa, lakini sijafurahishwa na hali ya uwanja, pamoja na baadhi ya maamuzi ya mwamuzi.

Kwa wachezaji wakubwa na ligi bora huwezi kucheza mpira kwenye uwanja kama huu, haikuwa mbaya kwa upande wetu, hata Coastal Union walikuwa wakipiga mipira mirefu, walijaribu kama mara mbili tatu kuanzia mpira nyuma wakashindwa na kuanza kubutua na hii si picha nzuri kwa Ligi ya Tanzania, kwangu mimi, Uwanja wa Azam Copmlex, New Amaan Zanzibar na Benjamin Mkapa, ndivyo vinavyobeba taswira njema ya ligi ya hapa nchini,“ alisema kocha huyo.

Hata hivyo, hakufafanua juu ya maamuzi mabaya ya waamuzi waliochezesha mchezo huo.

Akiuzungumzia mchezo huo, raia huyo ya Argentina, alisema kipindi cha kwanza hawakuwa bora, lakini walibadilika cha pili.

“Kipindi cha kwanza hatukutengeneza nafasi, lakini cha pili tulibadilika, nadhani mabadiliko tuliyoya-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042